# KUCHAMBUA MAUDHUI YANAYOPATIKANA KATIKA HADITHI ZA WATOTO KATIKA JAMII YA WAPEMBA

**MWANAIKA MADI MZEE**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA LA PEKEE LA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

**UTHIBITISHO**

Alietajwa hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo ***Kuchambuwa Maudhui ya Hadithi za Watoto Katika Jamii ya Wapemba***. Na nimependekeza ikubaliwe na chuo kikuu huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti la kutunukiwa Digirii ya M.A ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

____________________

Sheikh, Professa, Daktari, T. S. Y. Sengo

**(Msimamizi)**

____________________

Tarehe

## HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuigwa au kunakili kwa namna yoyote ile ya tasnifu hii kwa ajili yoyote kama vile kieletroniki, kurudufu nakala, kurikodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria kwa niaba.

# TAMKO

Mimi, **Mwanaika Madi Mzee** nathibitisha kuwa hiini kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chengine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyengine yoyote.

____________________

Saini

____________________

Tarehe

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mama yangu mpendwa Asha Maalim Hassan pamoja na baba yangu mpenzi Madi Mzee Omar kwa kunilea na kunipeleka shule. Mwenyeezi Mungu awabariki na kuwapa kila la kheri.

# SHUKURANI

Kwanza namshukuru Allah (s.w.) kwa kunijaalia siha njema na kuniwezesha kufika kiwango hiki cha elimu. Namshukuru Mungu kunijaalia misaada ya kitaaluma kutoka kwa wataalamu ambao sitoweza kuwataja wote.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Kiswahili wa OUT na SUZA kwa ushauri wao walionipa wakati wote nilipokuwa nikiandika tasnifu hii, waliniwezesha kuimarika kitaalimu, Mungu awabariki. Siwezi kuwasahau wahadhiri wetu wote walioshiriki katika kozi hii kama Professa Tigiti Sengo, Professa Emmanuel Mbogo, Professa James Mdee, muhadhiri Mohd Omary na wale wote waaliotusaidia katika kukamilisha kozi hii.

Shukurani za pekee zimwendee mshauri wa M.A.Kiswahili, tawi la Pemba Maalimu Bakari Kombo ambaye katowa mchango mkubwa tokea kuanza hadi kukamilika kwa kozi hii. Mungu amlipe kila la kheri kwawema huu usiopimika wala kulipika. Pia namshukuru mume wangu Ali Rajab Alikwakunivumilia hadi nikaikamilisha kuiandika tasnifu hii.

## IKISIRI

Kazi hii ilihusika na hadithi za Paukwa…. Pakawa. Imechunguza maudhui yanazopatikana katika hadithi za watoto katika jimbo la Mkanyageni Mkoa wa kusini Pemba. Ili kufikia lengokuu lililokusudiwa mbinu mbalimbali za utafiti zilihusika. Mbinu hizo ni za mahojiano pamoja na uchunguzi wa kimaktaba. Nadharia tatu za utafiti zilitumika. Nadhariza hizo ni mwitiko wa msomaji, nadharia ya simiotiki na nadharia ya sosholojia (kijamii).Kwa upande wa matokeo ya utafiti, mtafiti amegunduwa dhamira kadha wa kadha zilizoibuka kutokana na utafiti na uchambuzi alioufanya. Dhamira hizo ni ugumu wa upatikanaji wa elimu, umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. mapenzi na ndoa, kuonya,nafasi ya mwanamke, ukarimu, uzembe na uvunjaji wa kanuni pamoja na utawala bora. Kifani, mtafiti amegundua kwamba, baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira katika hadithi za watoto za Kipemba ni kipengele kinachohusu wahusika, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mandhari.Ujumbe uliojitokeza katika hadithi za watoto ni pamoja na wazee kuwaasa watoto juu ya kufuata ushauri wa  wazazi wao kwa kila wanalotaka kulifanya, kujitenga na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kukuletea vikwazo au matatizo, wanataalimu wawe wavumilivu, wasiwe na ufedhuli na lugha chafu kwa wanafunzi wao. Ujumbe mwengine uliopatikana ni kuwa na juhudi ya kazi na kuwacha kujigamba pasipo sababu, kutokuwa na imani na kila mtu,kuepuka ubinafsi na ujanja katika kazi, kutii kanuni na utii wa wake na waume zao na kuepuka ushawishi wa mashoga na watu wengine.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........................................................................................................ **ii**

**HAKI MILIKI** ........................................................................................................ **iii**

**TAMKO** ........................................................................................................ **iv**

**TABARUKU** ........................................................................................................ **v**

**SHUKURANI** ........................................................................................................ **vi**

**IKISIRI** ........................................................................................................ **vii**

**YALIYOMO** ........................................................................................................ **viii**

**VIFUPISHO** ………………………………...…………………………...……….**xiv**

**SURA YA KWANZA**........................................................................................................ 1

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA** ........................................................................ 1

1.1 Kitangulizi cha Kisiwa cha Pemba........................................................................ 1

1.2 Utangulizi wa Sura ........................................................................ 2

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti........................................................................ 2

1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti........................................................................ 6

1.5 Madhumuni ya Utafiti ........................................................................ 7

1.5.1 Madhumuni Mahususi ........................................................................ 8

1.5.2 Maswali ya Utafiti ........................................................................ 8

1.6 Umuhimu wa Utafiti........................................................................ 8

1.7 Mipaka ya Utafiti........................................................................ 9

1.8 Vikwazo vya Utafiti ........................................................................ 9

1.8.1 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti........................................................................ 10

1.9 Hitimisho ........................................................................ 10

**SURA YA PILI** ........................................................................................................ **10**

**2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ... 10**

2.1 Utangulizi wa Sura ........................................................................ 10

2.2 Dhana Mbalimbali Zihusuzo Mada ..... 11
2.2.1 Hadithi au Simulizi ..... 11
2.2.2 Fasili ya Ngano ..... 13
2.2.3 Dhana ya Fasihi ya Watoto. ..... 13
2.2.4 Aina za Hadithi ..... 16
2.2.5 Ngano ..... 17
2.2.6 Tarihi ..... 17
2.2.7 Visasili ..... 18
2.2.8 Vigano ..... 18
2.2.9 Soga ..... 18
2.3 Dhana ya Dhamira ..... 19
2.4 Uchambuzi wa Vipengele vya Fani ..... 20
2.4.1 Wahusika ..... 20
2.4.2 Mazingira ..... 20
2.4.3 Lugha ..... 21
2.5 Baadhi ya Vipengele vya Maudhui ..... 21
2.5.1 Ujumbeni ..... 21
2.6 Utalii wa Kazi Tangulizi ..... 21
2.7 Mwega wa Nadharia ..... 27
2.7.1 Maana ya Nadharia ..... 27
2.7.2 Sababu za Kuchaguwa Nadharia Hizo ..... 27
2.7.3 Nadharia ya Kijamii ..... 27
2.7.4 Nadharia ya Simiotoki ..... 28
2.7.5 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ..... 28
2.8 Hitimishoa ..... 29
**SURA YA TATU ..... 30**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI ..... 30**
3.1 Utangulizi wa Sura ..... 30
3.2 Maana ya Mahojiano ..... 30
3.2.1 Sababu za Kuchagua Mbinu ya Mahojiano ..... 30
3.2.2 Faida za Mahojiano ..... 30
3.2.3 Hasara za Njia ya Mahojiano ..... 31
3.2.4 Uteuzi wa Watafitiwa ..... 31
3.2.5 Jedweli la Watafitiwa ..... 31
3.3 Muundo waUtafiti ..... 32
3.4 Hitimisho ..... 32
**SURA YA NNE ..... 33**
**4.0 UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA ..... 33**
4.1 Utangulizi wa Sura ..... 33
4.2 Uchambuzi wa Data ..... 33
4.3 Dhamira Zilizopatikana Katika Hadithi Zilizokusanywa Katika Jamii ya Wapemba. ..... 33
4.3.1 Dhamira ya Ukaidi ..... 33
4.3.2 Dhamira ya Ujasiri ..... 34
4.3.3 Dhamira ya Malezi ..... 35
4.3.4 Dhamira ya Ushujaa ..... 35
4.3.5 Dhamira ya Uongozi Mbaya ..... 36
4.3.6 Dhamira ya Kusaidiana ..... 36
4.3.7 Dhamira ya Uchoyo ..... 37
4.3.8 Dhamira ya Kiburi ..... 37
4.3.9 Dhamira ya Kufanya Kazi ..... 38
4.3.10 Dhamira ya Subira ..... 39

4.3.11 Dhamira ya Makaazi ........................................................................... 39

4.3.12 Dhamira ya Ubinafsi .......................................................................... 40

4.3.13 Dhamira ya Urafiki ............................................................................ 41

4.3.14 Dhamira ya Uchoyo ........................................................................... 41

4.3.15 Dhamira ya Ujanja ............................................................................. 42

4.3.16 Dhamira ya Wizi naUbadhirifu wa Mali. ........................................... 43

4.3.17 Nafasi ya Mwanamke ......................................................................... 43

4.3.18 Dhamira ya Uzembe ........................................................................... 44

4.3.19 Dhamira ya Uvunjaji waSheria ......................................................... 45

4.3.20 Dhamira ya Unyonyaji ....................................................................... 46

4.3.21 Dhamira ya Utawala Bora .................................................................. 46

4.3.22 Dhamira ya Umoja na Mshikamano ................................................... 47

4.3.23 Dhamira ya Mapenzi na Ndoa ............................................................ 47

4.3.24 Dhamira ya Uhalifu ............................................................................ 48

4.4 Ujumbe Uliopatikana Katika Hadithi Zilizokusanywa Katika Jamii ya Wapemba ..................................................................................................... 49

4.5 Vipengele vya Fani Vilivyosaidia Kuibuwa Dhamira Katika Hadithi za Watoto Katika Jamii ya Wapemba……………………..……………..…….52

4.5.1 Wahusika ............................................................................................ 53

4.5.1.1 Mhusika Pate. ..................................................................................... 53

4.5.1.2 Mhusika Mize ..................................................................................... 53

4.5.1.3 Mhusika Mwengine ni Zimwi ............................................................ 53

4.6 Katika Hadithi ya 2ya Chura na Jingoo Kuna Wahusika Wafuatao .................. 54

4.6.1 Chura .................................................................................................. 54

4.6.2 Jongoo ................................................................................................. 54

4.7 Katika Hadithi ya 3 ya Makame wa Makame Kuna Wahusika Wafuatao ......... 55

4.7.1 Makame wa Makame ........................................................................... 55

4.8 Katika Hadithi ya 4 ya Paka na Panya Kuna Wahusika Wafuatao .................. 55

4.8.1 Panya ........................................................................................... 55

4.8.2 Paka ............................................................................................ 55

4.9 Hadithi ya 5 ya Sungura ina Wahusika Wafuatao............................................ 56

4.9.1 Nfaki ........................................................................................... 56

4.9.2 Sungura ........................................................................................ 56

4.10 Katika Hadithi ya 6 ya Fisi na Simba Tumewaona Wahusika Hawa Wafuatao ........................................................................................... 57

4.10.1 Simba ......................................................................................... 57

4.10.2 Fisi ............................................................................................ 57

4.11 Katika Hadithi ya 7 ya Kungu Mauwa kuna Wahusika Wafuatao .................. 57

4.11.1 Mwau ......................................................................................... 57

4.11.2 Lau ............................................................................................ 58

4.12 Hadithi ya 15 ya Muhamedi ina Wahusika Hawa:........................................... 58

4.12.1 Muhamedi .................................................................................... 58

4.13 Katika Hadithi ya 9 ya Yamuimui inaWahusika Hawa Wafuatao:.................... 59

4.13.1 Yamuimui .................................................................................... 59

4.13 Hadithi ya 12 ya Babu Dii Imetupatia Wahusika Hawa Wafuatao:................... 59

4.13.1 Babu Dii. ..................................................................................... 59

4.13.2 Mke wa Babu Dii. ......................................................................... 59

4.13.1 Bibi Kizee. ................................................................................... 60

4.14 Katika Hadithi ya 13 ya Kijoka Kuna Wahusika Hawa .................................. 60

4.14.1 Mama Yake Kijoka......................................................................... 60

4.15 Hadithi ya 14 ya mtu na ndugu yake wahusika Waliomo ni ............................ 61

4.15.1 Binadamu .................................................................................... 61

4.15.2 Simba ........................................................................................................ 61

4.16 Hadithi ya 10 ya Bunuasi na Wafuatao ........................................................... 61

4.16.1 Bunuwasi ................................................................................................... 61

4.7 Matumizi ya Lugha Katika Hadithi Teule za Wapemba. ................................. 62

4.7.1 Tamathali za Usemi ..................................................................................... 63

4.7.4 Takriri ........................................................................................................ 64

4.7.5 Tanakali Sauti............................................................................................. 64

4.7.6 Taswira ...................................................................................................... 64

4.7.7 Methali ....................................................................................................... 65

4.8 Mandhari ..................................................................................................... 65

**SURA YA TANO ………………………..……………………………….……...….. 67**

**5.0 HITIMISHI, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO.................................. 67**

5.1 Utangulizi wa Sura ........................................................................................ 67

5.2 Hitimishi ..................................................................................................... 67

5.3 Muhutasari wa Utafiti .................................................................................... 68

5.3.1 Matokeo ya Utafiti........................................................................................ 68

5.4 Mapendekezo ............................................................................................... 69

**MAREJELEO …………………………………………………….………...….. 70**

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| OUT | : | The Open University of Tanzania |
| SUZA | : | The University of Zanzibar |
| TUKI | : | Taasisi ya Ukuzzaji Kiswahili |
| TALILUKI | : | Taasisi ya Kiwahili na Ligha za Kigeni |
| S.W | : | Subhanna Wataala |
| M.A. | : | Master of Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1 Kitangulizi cha Kisiwa cha Pemba

Kisiwa cha Pembakina mapisi marefu.Kwa upande wa jina la kisiwa inasemekana kuwa linatokana na neno la Kiswahili “kupemba”kwa maana ya kuongoza chombo kwa umakini. Fasili hii inatokana na hali ya kisiwa cha Pemba kuzungukwa na mkondo mkubwa na wenye hatari.Pemba ikiitwa Al-jaziratul hadhara “kwa maana ya kisiwa cha kijani kutokana na rutuba ya ardhi yake na kukifanya kisiwa kuwa bustani nzuri (Krain 1998).

Maulid (2011) anadai kwamba “Msumbiji kuna Pemba,hivyo Wapemba waliletwa kwa wingi kisiwani Pemba na hao hasa ndio walioleta jina hilo na herufi “n”katika Kiswahili chakisiwani Pemba, badala ya “m,” kwa mfano neno “nkate”badala “mkate”.Sengo (1985), anasema kwamba Pemba ni kizushi cha volkano, kilizushwa kutoka chini ya bahari.Kijiografia:katika mwelekeo wa kaskazini na kusini mwa dunia kisiwa cha Pemba kipo upande wa kusini mwa mstari wa ikweta.Na mwelekeo wa magharibi na mashariki kimepakana baina ya kilomita 30-50 nje ya ufukwe wa Tanganyika katika mwambao wa Afrika ya mashriki.Kisiwa cha Pemba kina eneo la ukubwa wa kilomita 863 za mraba. (Omar 2011).

Kwa hiyo, mtafiti anaona, kutokana na udogo wa kisiwa cha Pemba, hapo kale jamii ya Wapemba iliweza kushirikiana katika suala la malezi ya watoto wao, na malezi hayo yaliweza kufikishwa kwa watoto kwa njia mbalimbali, ikiwemo kuwakusanya watoto na kuwasimuliya hadithi za paukwa ……pakawa. Dhamira zilizokuwemo katika hadithi hizo,ziliwafunza watoto mambo mengi, ikiwa ni pamoja na jinsi ya kuishi katika jamii

zao, kuwatii wazee wote na kujifunza amali za jamii zao, ili waweze kufuata mila na desturi za jamii zao.

## 1.2 Utangulizi wa Sura

Katika kipengele hiki tunazungumzia kitangulizi cha kisiwa cha Pemba,tatizo la utafiti, usuliwa tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia mtafiti ameelezea umuhimu wa utafiti, eneo la utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti, tamko la tatizo la utafiti, sababu za kuchaguwa mada na utatuzi wa vikwazo vya utafiti.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Katika utafiti huu,mtafiti amekusudia kuainisha maudhi katika vipegele vya dhamirana ujumbe wa hadithi za watoto katika jamii ya wapemba. Masimulizi ya hadithi za watoto ni moja miongoni mwa vijipera vya fasihi simulizi. Kuhusiana na mada ya fasihi simulizi,Mulokozi (1996) anaeleza kuwa fasihi simulizi imekuwa na umuhimu mkubwa katika jamii,ikiwemo haja ya kuelimisha jamii juu ya masuala yanayofaa kufuatwa na yale yasiyofaa kufuatwa, ili jamii iweze kuwa katika mwenendo bora wa kimaisha. Kwa kuwa hadithi za watoto ni kijitanzu kidogo cha fasihi simulizi, mtafiti ameona ipo haja ya kuidokeza dhana ya fasihi simulizi, ingawa kwa ufupi.wataalamu waliotowa maoni kuhusu maana ya fasihi simulizi miongoni mwao ni Finnegan(1970), Metteru (1989), Balisidya (1983), Sengo (1985), naOkpwho (1992).

Matteru (1989), anasema kwamba fasihi simulizini fasihi inayotegemea mdomo, njia mojawapo ya kutolea na kuenezea elimu. Balisidya (1983), fasihi simulizi ni elimu ya kifasihi ambayo hutumia mdomo au njia nyengine katika kuwasilisha na kusambaza elimu kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Kama anavyoainisha Okopwho (1992), fasihi simulizi ni elimu itolewayo kwa neno la mdomo. Mawazo hayo yote yanaweza kuhitimishwakwa kauli ya Mulokozi(1996), fasihi simulizi ni maneno ya sanaa tendezi,

ambayo huwasilishwa kwa njia ya mdomo na kuhifadhiwa kwa maandishi, flash, CD, sahani za santuri, kanda za kurikodi na njia nyengine za kuhifadhi elimu hiyo.

Mulokozi, ameainisha tanzu za fasihi simulizi katika makundi sita, ambayo ni mazungumzo, ushairi, semi maigizo na masimulizi (1989). Hadithi kama moja ya kitanzu cha tutumbi au nathari, kinaelezwa kwa uainishaji wake kwa kuwa ni cha muda mrefu, Kwa mujibu wa Okpewho (1982), kuna vigezo au njia nne, na katika hizo ndizo mpaka sasa zimetumika kuainisha hadithi. Kwavile mtafiti data zake alizipata moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa wake, aliona ni bora kuvianisha vigezo hivyo kama vifuatavyo:
Kigezo cha kwanza ni kigezo cha unguli, katika kigezo hicho kunajitokeza ngano zihusuzo mwanadamu na ngano za Miungu. Pili ni kigezo cha lengo la ngano inayohusika, katika kigezo hichi ngano zinaainishwa kwa kuzingatia lengo la usimulizi, kama vile ngano za kimaadili na ngano za kuhimiza kazi, kundi kubwa la ngano ni zile za kimaadili.Tatu ni kigezo cha sifa na ubora wa ngano, kigezo ambacho ndicho kinachoonekana kubeba kundi kubwa la ngano. Katika kigezo hiki kuna ngano ambazo huambatana na uerevu au ulaghai wa wahusika.

Ngano za kihistoria ambazo huhusu vita, vizazi, mashujaa, usuli wa kitu au jambo fulani Nne ni kigezo cha muktadha wa utendaji wa ngano, katika kigezo hichi kinachoangaliwa zaidi ni ngano inatendwa wakati gani na katika mazingira gani. Kwa mfano, kwa kutumia kigezo hiki, tunaweza kupata hadithi zinazotendwa wakati wa mbalamwezi, ngano zinazitendwa wakati wa ibada, wakati wa misiba na hata wakati wa mavuno, kama ilivyo katika jamii za kipemba wakati wa mavuno ya karafuu watu husimuliana hadithi wakati wakiwa wanachambuwa karafuu kwa lengo la kuwa wachambuzi wasichoke wala wasisinzie.

Utanzu wa fasihi ambao umekuwa ukipewa umuhimu mmojawapo ni huo wa hadithi, katika kitanzu cha hadithi za watoto, matendo yanayooneshwa na wahusuka hujenga mtiririko wa vituko vinavyokamilisha hadithi hiyo. Wahusika katika hadithi wanaweza kuwa ni binadamu na viumbevyengine vyovyote, ambavyo vimepewa sifa za kibinadamu. Viumbe hivyo, hujenga zaidi, dhamira iliyokusudiwa na kuchaguliwa kutokana na tabia za viumbe hivyo. Kwa mfano, mnyamakama Simba, huwakilisha dhanna ya ukali, Sungura huwakilisha ujanja,fisi huwakilisha woga na tamaa, pia zimwi na shetani huwakilisha dhanna ya viumbe vinavyotisha Hamad (1981).Hamad (keshatajwa) anaendelea kusema, hadithi hizo aghalabu huwa ni fupifupi, hivyo hutumia muundo wa moja kwa moja ili zieleweke kwa urahisi. Katika hadithi hizo za jadi, fanani pia,ana nafasi katika kufikisha ujumbe, kwani hupata fursa ya kushiriki katika utambaji wa hadithi.

Pia hadithi za aina hiyo, hutumia nyimbo ambazo husaidia sana kufikisha ujmbe kwa hadhira, vilevile nyimbo hutumika kuwaburudisha wasikilizajiHamad(ameshatajwa). Hamad anaendelea kwa kusema,hadithi chanzo chake katika jamii ni makuzi na walezi kuishi pamoja katika miji na vitongoji kutokea asili, watu walipoanza kutumia lugha ya fasihi kama ni chombo cha mawasiliano .

Nivigumu kwa mtafiti yoyote kuweza kuthibitisha kama aliweza kumpata mzeealiyeweza kukumbuka tarehe maalumu na pahala pamojawapo palipoanza sanaa hii.Wengi walisema, fani hii ni moja kati ya jumla ya mazungumzo ya maana ambayo mara nyingi huwa ni mchanganyiko wa wazee nawatoto kukutana na kutambiana hadithi kwa shabaha yakutahadharishana,kushauriana,kuonyana na kuelezana mambo muhimu yanayohusu maisha yao. Kutokana na mfumo wa jadi hadithi mara zote, zilitolewa nyakati za jioni, aghalabu baada ya sala za magharibi na isha. Zama hizo, ilikuwa ni marufuku au ni mwiko kutambiana hadithi mchana kwa sababu ya harakati za kimaisha.

Japo kuwa mwiko ulikuwa na siri za kimsingi,hapo kale,mpaka leo unaumuhimu, pamojana maendeleo ya kisasa. Katika madrasa hasa ya msingi, ipo dharura ya kuwatolea watoto hadithi na wao kutambiana hadithi zao mchana. Hii ni njia, miongoni mwa njia za kuendeleza mafunzo kwa jumla. Maelezo hayo yanaonyesha chimbuko la haditi katika jamii za kale. Hadithi katika misingi yake ya maana ni hisia za jamii katika kulea na kuadilisha jamii. Mtoto katika jamiiyake alijengwa kuamini kuwa mzee (mtumzima) hakosei na iwapo baba wa mtoto kakosea mtoto hamwambii baba yake hivyo waziwazi atatumia mbinu inayostahiki, kama kusema alimsia babu fulani akisema kufanya jambo fulani ni vibaya na halifai katika jamii yetu. Huku akiwa na lengo la kumkosoa baba yake na haya ni mafunzo yaliyotokana na hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba.

Ndungo na wenzake (1991), wanaeleza kuwa utanzu huo ulikuwa na madhumuni ya kusimulia hadithi au kutamba hadithi.Lengo mahsusi la kusimulia hadithi ni kuburudisha au kutumbuiza wasikilizaji.Utanzu huo ulipitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njiya ya mdomo. Utunzi wake, kinyumena hadithi za kileo, haujuilikani, yaani hakuna mtu aliyeweza kusemwa ni hadithi ya mtunzi huyu au yule. Ni masimulizi ambayo nimali ya jamii nzima na kwa hivyo hazikumilikiwa na mtunzi yeyote.

Umuhimu wa hadithi za paukwa….pakawa, ulikuwa katika kuendeleza na kuhifadhi maadili na mienendo ya jamii. Hadithi ilipotungwa kila mtu alikuwa huru kuisimulia kwawengine. Hakuna hadithi iliyotungwa mara mbili tatu ikabakia ilivyo, kila ilipotambwa ilkuwa ngeni naya kipekee.

WWW.gafkosft.com/ walisema kuwa hadithi huwa na mianzo maalumu yaani huwanza kwa;

Paukwa…..pakawa au hadithi…..hadithi,hadithi njoo…,hapo zamani za kale ………

Pia, wamesema hadithi huwa na miishio maalumu. Mfano,hadithi yangu yaishia papo….,wakaishi raha mustarehe. Hadithi hizo zilikuwa na umuhimu wake,mfano kuhifadhi au kurithisha amali za jamii. Kuelimisha au kutoa mafunzo kuhusu jambo maalumukupitisha muda, hasakwa watoto waliposubiri chakula kiive. Kwa mujibu wa Muhamed na wenzake (1981), hadithi za watoto ni utanzu wa karne na karne,ambao mwanadamu na wataalamu kadhaa, wamewahi kufanya utafiti juu ya ngano.Kwa mfano, Finnegan (1970), Sengo (1985), Mulokozi (1986),Senkoro (1997), Okpewho ni miongoni mwa wataalamu waliowahi kutafiti hadithi simulizi na kufafanua vipengele kama vile, ngano, tendina visasili katika maudhui na fani. Hata hivyo, baada ya kutalii maandishi imegundulikana kuwa hakuna uchunguzi wa dhamira za hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba, uliowahi kuandikiwa. Kwa muktadha huo mtafiti wa kazi hii ameamuwa kulitupia macho eneo hili ili kuziba pengo hilo la utafiti ambalo ni kuchambuwa maudhui katika vipengele vya dhamira na ujumbe za hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba.

## 1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Tatizo la tamko la utafiti ni kuchunguza maudhi katika vipengele vya dhamira na ujumbe katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Mtafiti katika kusoma kwake tasnifu mbalimbali aliona kuna waandishi wachache walioandikia kuhusu hadithi simulizi za Zanzibar, ambao niSenkiwa (1974), Haji na wenzake (2007), Said (2005), na Omar (2013).Senkiwa (1974), alikusanya hadithi tisa za kienyeji katika jamii za waswahili, ambazo jamii ziliwasimulia watoto wao mara kwa mara. Madhumuni ya kukusanya hadithi hizo, ilkuwa ni kudumisha utamaduni, elimu na maarifa ya babu zetu, yaani mawazo yao kuhusu maisha. Mtafiti huyu alichunguza zaidi vipengele vya matumizi ya lugha, kama vile methali zinavyomsaidia mtoto kuipenda na kuitumia lugha yake. Pamoja na kuwa mtafiti huyu utafiti wake ulihusu hadithi, lakini alionekana

kushughulikia zaidi vipengele vya fani, kama vile matumizi ya lugha. Na hakujihusisha na uchunguzi wa dhamira katika hadithi hizo. Haji na wenzake (1974), walichunguza mafunzo yanayopatikana katika hadithi za jamii ya Watumbatu, waligundua mafunzo kama vile, ukiomba dua usiombe kwa maneno ya ovyo, mja ikiwa atajiegemeza kwa mwenyezi Mungu kikweli si rahisi kufikwa na matatizo ya kidunia.

Watafiti hawa utafiti wao ulielekea katika hadithi za jamii ya Watumbatu na hawakujihusisha na uchunguzi wa maudhui katika jamii ya Wapemba. Said (2005), alitafiti mafunzo ya hadithi za pukwa – pakawa katika jamii ya Wazanzibar, na akaibuwa mafunzo mbalimbali. Lakini mtafiti huyu nae, alitafiti zaidi mafunzo ya hadthi katika jamii ya watu wa Unguja. Na hakuangalia maudhui katika hadithi za jamii ya Wapemba. Omar (2013), aliandika juu ya nafasi ya hadithi simulizi katika kumfunzamtoto maadili mema katika skuli za upili, visiwani Zanzibar. Miongoni mwa malengo yake, ni kuchunguza mbinu mpya za kufundishi hadithi kwa urahisi katika shule za upili visiwani Zanzibar.

Pia mtafiti huyu hakuwa na malengo ya kuchunguza maudhui ya hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Kutokana na mapitio hayo mtafiti ameona hakuna tasnifu yoyote iliyojikita kuandikia juu ya uchambuzi wa maudhui ya hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Kwa hivyo, mtafiti wakazi hii alichunguza maudhui ya hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba ili kuziba pengo hilo la utafiti lililoachwa na watangulizi hao.

### 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguzana kuchambuwa maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya wapemba.

### 1.5.1 Madhumuni Mahususi

1.5.1.1Kubainisha dhamira zilizojitokeza katika hadithi za watoto za paukwa ……pakawa katika jamii ya Wapemba.

1.5.1.2 Kuchunguza ujumbe uliojitikeza katika hadithi za watoto zilizoteuliwa katika jamii ya Wapemba.

1.5.1.3Kubainisha baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira za hadithi za watoto katika jamii ya wapemba.

### 1.5.2 Maswali ya Utafiti

1.5.2.1 Ni dhamira zipi zilizojitokeza katika hadithi za watotoza jamii ya Wapemba?

1.5.2.2 Ni ujumbe gani unaopatikana katika hadithi za watoto zinazosimuliwa katika maisha ya kila siku?

1.5.2.3 Je ni vipengeale vipi vya fani vinavyosaidia kuibuwa dhamira za hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu wa hadithi za watoto umeonekana kuwa na umuhimu kama ufuwatao: Utafiti huu utawasaidia wataalamu wa fasihi wakiwamo maprofesa, wahadhiri, walimu na wanafunzi kupata data muhimu zinazohusu hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Pia utafiti huu utawasaidia wale ambao watataka kufanya utafuti katika uwanja huu wa hadithi za watoto ili kupata marejeleo kutokana na mada watakazozifanyia kazi.

Vile vile, utafiti huu utatowa nafasi ya kuongeza maarifa ambayo itapeleka mbele taaluma ya fasihi. Kwani utafiti huu umetumia nadharia mbalimbali, ambazo zimechambuliwa na kutumiwa katika uchambuzi wa dhamira, ujumbe na baadhi ya

vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira tafauti zilizojitokeza katika tasnifu hii. Utafiti huu utatumika kama marejeleo kwa wanafunzi na walimu wa fasihi. Wanafunzi wa fasihi watajifunza na kuona dhamira zilizojitokeza katika hadithi za watoto. Kwa hivyo, hata wasomaji katika masomo mengine, yakiwemo ya sayansi jamii, wataweza kujifunza kutokana na tasnifu hii katika kujiendeleza kitaalimu.

### 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa maudhui katika hadithi za watoto kisiwani Pemba. Mtafiti aliangalia vipengele kama vile dhamira, ujumbe na kuangalia baadhi ya vipenge vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira katika hadithi teule.Hadithi zilizochaguliwa na kufanyiwa uchunguzi ni hadithi za watoto za kijadi. Hadithi zilizokusanywa, zimetoka kwa watoto na wazee wa vijiji vya Shidi, Mkanyageni na Michenzani, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa kusini, Pemba. Mtafiti hakujihusisha na maeneo mengine kutoka katika kisiwa cha Pemba na hakujihusisha na hadithi zilizoandikwa katika vitabu vya watoto, bali alijikita na hadithi za masimulizi ya mdomo ya moja kwa moja.

### 1.8 Vikwazo vya Utafiti

Inaonekana utanzu huu wa hadithi za watoto, katika kuangalia maudhui, katika jamii ya Wapemba bado haujafanyiwa utafiti kwa kiwango kikubwa kama zilivyofanyiwa tanzu nyengine za fasihi.kwa hivyo kuna shida kidogo ya kupata kusoma kazi tangulizi nyingi kama mtafiti alivyotarajia. Pia watafitiwa ni watu wanaoishi karibu na mazingira ya pwani, muda mwingi walikuwa katika shughuli zao za uvuvi, kwa hivyo, baadhi yao mtafiti aliwakosa kwa muda aliofika katika eneo la utafiti, na ilibidi mtafiti arudi tena kwa kuwafuata watafitiwa baada ya kurudi katika harakati zao za kimaisha kitu ambacho kilisababisha kuzorota kwa ratiba ya utendaji wake.

### 1.8.1 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti

Ili kuvitatuwa vikwazo ambavyo mtafiti alikabiliana navyo katika utafiti wake, alitalii kazi tangulizi zilizohusu mada yake katika mitandao na kuwafuata baadhi ya wataalamu na wanafunzi ambao tayari wameandika tasnifu zilizowiana na mada yake. Pia mtafiti alitembelea maktaba ili kutalii kazi ambazo zinamfanano na kazi aliyoandikia. Kuhusu kuwapata watafitiwa, mtafiti aliwafuata kulingana na fursa yao ya kupatikana hasa nyakati za jioni.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura ya kwanza mtafiti aliangalia usuli wa tatizo la utafiti, kwa kuzungumzia historia fupi ya hadthi za watoto. Pia akaelezea tamko la tatizo la utafiti kwa kurejelea watafiti ambao waliandikia kuhusiana na mada yake. Vilevile alishulikia malengo ya utafiti, ambayo yalihusisha malengo makuu na malengo mahususi. Yakifuatiliwa na maswala matatu ya utafiti. Umuhimu wa utafiti nao ulionyeshwa katika vipengale viwili, ambavyo ni umuhimu kwa wasomaji wa fasihi na umuhimu wa kinadharia. Mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo vya utafiti pia navyo viliangaliwa.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi wa Sura

Sura ya pili imezingatia utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, imeelezea maana ya nadharia na kufafanuliwa nadharia kama vile, nadharia ya nadharia ya kijamii,

nadharia ya simiotiki na nadharia ya mwitiko wa msomaji. Dhana mbalimbali zihusuzomada zimefafanuliwa, ikiwa ni pamoja na dhana ya hadithi similizi, fasili ya ngano, dhana ya fasihi ya watoto, aina za hadithi na dhana ya dhamira.

## 2.2 Dhana Mbalimbali Zihusuzo Mada

### 2.2.1 Hadithi au Simulizi

Hadithi ni simulizi za kinathari au kitutumbiambazo huwa na wahusika ambao huzungumziwa katika hadithi hiyo. Wahusika katika hadithi za fasihi wanaweza kuwa ni wanadamu au viumbe vyovyote vilivyopewa sifa au uwezo wa kibinadamu. Hamad na wenzake(1981). Hadithi katika fasihi simulizi, aghalabu huwa ni fupi fupi, hivyo hutumia mtindo wa moja kwa moja ili ieleweke kwa urahisi. Katika maelezo hayo ya utambaji wa hadithi fanani pia, ana nafasi ya kufikisha ujumbe kwani hutegemea namna alivyo na uwezo wa kuelezea kwa kutumia viungo vyake vya mwili mbali na kutumia maelezo. Aidha, hadithi hutumia mbinuya nyimbo. Mbinu hii husaidia kufikisha ujumbe kwa hadhira na kuwaburudisha wasikilizaji.

Hadithi, kwakawaida, huwa na vianziovyake, kianziomashuhuri ni kile cha paukwa....pakawa. Hamad na Wenzake (1981), kianzio hiki ndio kilicho maarufu sana miongoni mwa hadithi za kitoto katika kisiwa cha Pemba.Vianzio vyengine vinavyotumika ni kama vile Hadithi…hadithi…hadithi njoo, utamu kolea….hapo zamani za kale….Vianzio hivi kazi yake kubwa, ni kuitayarisha hadhira kuwa tayari kusikiliza na kuchangia.

Hadithi, kama zilivyo tanzu nyengine za fasihi,huwa na sifa zake bainifu, zifuatazo ni miongoni mwa sifa hizo: Hueleza matukio katika mpangilio fulani mahususi.Maranyingi hadithi za fasihi simulizi huwa nampangilio wa moja kwa moja. Inawezekana,ni kutokana na ukweli kwamba mara nyingi huwalenga watoto ambao uwezo wao kwa kuunganisha matukio ni mdogo kulingana na umri wao.Huwa na wahusika,yaani

watendaji au watendwaji katika matukio yanayosimuliwa. Wahusika hao wanaweza kuwa binadamu, majini, vitu, mwahala au kiumbe chochote kinachojulikana au kiumbe cha kinadharia kinachopewa sifa za kibinadamu. Hutumia lugha ya kimaelezo. Lugha hiyo, wakati mwengine huchanganywa na mazungumzo. Lakini pia, wakati mwengine, lugha ya ushairi hutumika, hasa pale matumizi ya mbinu ya nyimbo inapotumiwa.Kwa kawaida, lugha ya hadithi hupambwa kwa mbinu za matumizi ya lugha, kama vile, tamathali za semi na lugha za picha na ishara.

Utambaji wake huambatanana na vitendo au ishara. Katika sifa hii, umahiri wa fanani na ubora wa hadhira unamchango mkubwa katika kuiremba hadithi ya fasihi simulizi. Ni kwa sifa hii, ndiyo husemwa, uwasilishaji wa fasihi kwa njia ya masimulizi husemwa kuwa ni hai na wenye kusisimua zaidi kuliko uwasilishaji wa kutumia maandishi. Huwa na maudhui ya kweli au ya kubuni na yenye mafunzo fulani kwa jamii.Maudhui ya hadithi za fasihi simulizi maranyingi, huwa ya kufunza,kuadabisha, kuelimisha, na kounya. Kwa mfano huifunza jamii juu ya kufuata mwenendo mzuri unaokubaliwa na jamii yao au kuionya jamii kuachana na mambo yasiyokualika kulingana na mila na desturi za jamii husika. Maudhui haya marazote huendana na utamaduni wa jamii, ambamo, hadithi imebuniwa. Kwa mnasaba huo, uundaji wa maudhui ya hadithi za fasihi simulizi ni miongoni mwa sifa bainifu zinazokipambanua kitanzu hiki.

Ndungo na Wangari ([1991), wametoa, maana ya hadithi kwa kuwaunga mkono, Hamad na wenzake, kwa kusema kwamba ni simulizi za kinathari.Lengo mahususi la kusimulia hadithi ni kuburudisha au kutumbuiza wasikilizaji au hadhira, kwa mfano wazee baada ya kumaliza shughuli za mchana kutwa, hukaa na watoto wao kuwasimulia hadithi kama ni sehemu ya kuwaburudisha watoto na kuwafurahisha. Hata hivyo, Wangari na Ndungo (wameshatajwa) wanaelezea, hadithi pia ina dhima ya kufundisha,

kuonya au kukosowa jamii. Inafaa tukumbuke kwamba mtindo huowa kusimulia hadithi ulitumiwa sana kwa njia ya kuelimisha jamii hususani vijana, hasa katika malezi na mienendo bora wazee walitumia mtindo huu kuwaelimisha vijana kuhusu amali za jamii zao.

### 2.2.2 Fasili ya Ngano

Wataalam mbali mbali wametoa maelezo kuhusu maana ya ngano.Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) "ngano ni hadithi fupi ambazo wazee huwasimulia aghalabu watoto". Wazee inaonekana walikuwa hawafanyi hivyo kwa bahati mbaya bali walikuwa wakiwasimuliawatoto ngano hizo ikiwa kama ni sehemu ya kutowa mafunzo kwa watoto. Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa "ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo huwatumia wahusika wa aina mbalimbali wakiwemo wanyama, miti au watu kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo. Mafunzo katika hadithi hubebeshwa wahusika hao ili kusadifu hali halisi inayohusu jambo linalozungumzwa katika hadithi hizo. Neno 'ngano' hutumiwa katika jamii zetu kwa maana pana sana kiasi kwamba aina nyingine ya simulizi au hadithi zinaweza kujumlishwa kwenye kundi pana la ngano. Nao Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayo kumbana nayo ulimwenguni.Matatizo hayo yanaweza kuwa ya kijamii, kiuchumi au kisiasa, mradi tu yamemgusa mwanadamu.

### 2.2.3 Dhana ya Fasihi ya Watoto.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), fasihi ya watoto, ni fasihi ambayo, imekusudiwa watoto. Kwa maana hiyoili kuhakikisha kuwa, fasihi hii imekuwa na mvuto kwa watoto, ni lazima fasihi hiyo iweze kufanikisha kuiteka saikolojia ya watoto.  Anaendele kusema kuwa, fasihi ya watoto ni fasihi maalumu, kwa ajili ya watoto.

Maelezo haya ya Wamitila, yametupa ufafanuzi fulani, juu ya fasihi ya watoto, ambapo, ufafanuzi huo umetusaidia kupeleka mbele utafiti wetu huu, kwa mfano tumeweza

kuzichambuwa hadithi kwa kuzingatia jinsi mtoto anavyojifunza kutokana na hadithi aliyosimuliwa au kusimuliya, ingawa wao wanaelezea fasihi ya watoto iliyoandikwa lakini maelezo hayo angalau yametupatia muelekeo fulani unaohusu fasihi ya watoto. Hata hivyo, bado maelezo hayo hayajaweka wazi juu ya vipengele muhimu ambavyo vinapaswa kuwamo katika fasihi ya watoto, na hasa katika dhamira za hadithi za watoto.

Kwa hivyo ukiangalia dhana hii kwa mtaalamu huyu, utaona kuwa fasihi ya watoto ni dhana inayorejelea fasihi inayowahusu watoto pekee. Katika ufafanuzi wake,anaendelea kuelezea kuwa, fasihi ya watoto, huweza kuwa,ushairi, natiki, ambazo zimetungwa kwaajili ya watoto wadogo. Vile vile,anaelezea kuwa, fasihi ya watoto inajikita katika mambomakuu matatu. Jambo la kwanza, ni kuwa, muhusika mkuu, lazima awe ni mtoto au kijana, pili, dhamira lazima ziwahusu watoto na tatu, lazima fasihi ya watoto iwe na lugha iliyorahisi. Maelezo hayo yanakubalika kwa upande mmoja kwani, yamejaribu kudokeza, ni namna gani fasihi ya watoto inatakiwa iwe katikakipengele cha lugha, wahusika na hata dhamira. Bado utafiti unatakiwa uonyeshe dhamira za hadithi za watoto kinagaubaga katika eneo na uhalisia wa hadithi zenyewe. Baadhi ya hadithi za watoto, zipo ambazo hazina wahusika watoto. Aidha baadhi ya wahusika katika fasihi nyengine za watoto huwa ni wanyama, ambao kamwe hawajabainishwa kwamba ni watoto. Katika jamii za Waswahili zipo hadithi nyingi ambazo zina wahusikakama vile sungura, fisi, simba, chui, paka, nyani na zimwi. Vile vile, dhamira za fasihi za watoto huweza kuwahusu watuwazima. Kwa hivyo, dhamira tutakazozijadili zitawahusu watu wazimana watoto ingawa huweza kujitokeza zile zinazohusu watoto tu. Hili si jambo geni kwani watoto ni miongoni mwa kundi jamii.

Pia Wamitila (ameshatajwa) anaendelea kwa kusema, fasihi ya watoto na vijana lazima iwe inaonesha matendo na maisha ya muhusika waziwazi. Muhusika, lazima awe anatia hamasa na lazima kazi hiyo iwe inaburudisha. Kwa jumla, Wamitila (ameshatajwa)

anasema kuwa, saikolojia ya watoto na vijana huwa na maana ya mambo yote, ambayo, yanakuwamo katika kazi hiyo ili kuweza kuifanya kazi hiyo ya kuwavutiya vijana. Ili kufanikisha kuiteka saikolojia ya watoto na vijana, mambo yafuatayo ni vyema yaweze yazingatiwe.

a. Kazi hiyo,ni lazima iwe na mtazamo wa watoto na vijana ambao ni tafauti na watu wazima. Hivyo kufanikiwakwa mwanafasihi, ni pale ambapo, kazi hiyo itaendana na fikra za watoto.

b. Kazi iwe na lugha rahisi inayoendana na hadhira ya watoto na vijana. Miundo mengine na sentensi ngumu hazipendekezwi kutumika katika fasihi ya watoto na vijana isipokuwa kama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

c. Pia mwanafasihi anapaswa kuandika mada inayovutia watoto.

d. Vile vile, mwanafasihi anapoiandikia hadhira ya watoto lazima hadithi yake iwe fupi na ya kiutendaji, kwani kazi ndefu huwachosha watoto.

e. Mwanafasihi anapowachora wahusika, lazima kuwachora kuwa na mhusika mwema na mhusika muovu kwani hali hiyo huwavutia sana watoto.

f. Katika fasihi za watoto, wahusika wanyama wapewe nafasi za wahusika binaadamu kwani hali hii huwavutia watoto.

g. Kazi za watoto na vijana ni vyema ziwe za michezo, kwani, watoto hupenda sana michezo.

Maelezo hayo yaWamitila (ameshatajwa) yamepiga hatua kubwa katika kueleza sifa bainifu zinazohusu hadithi za watoto. Maelezo hayo yametusaidiaSana katika uchambuzi wetu, kwani yametupa mwanga wa namna ya kuzipata dhamira katika hadithi za watoto.

### 2.2.4 Aina za Hadithi

Kwa mujibu wa Ndumbaro (2013), naOkpewho (1970), uainishaji wa aina za hadithi ni tatizo la muda mrefu Okpewho (ameshatajwa) vigezo vine hutumika katika kuainisha hadithi.Vigezo hivyo ni kama hivi vifuatavyo:

Kwanza, kigezo cha unguli.Katika kigezo hiki, kunajitokeza ngano zihusuzo wanadamu, wanyama, na ngano za miungu. Pili, kigezo cha lengo la ngano. Katika kigezo hiki, ngano huainishwa kwa kutegemea lengo la simulizi. Hapa panajitokeza ngano za kimaadili, ngano za kuhimiza kazi. Okpewho anaelezea kuwa, katika kigezo hiki, kundi kubwa la ngano ni zile za kimaadili. Tatu, kigezo cha sifa za ubora wa ngano, kigezo ambacho ndicho kinachoonekana kubeba kundi kubwa la ngano. Katika kigezo hiki, kuna ngano ambazo huambatana na ujanja, uerevu wa wahusika, mtanziko, na ngano za kihistoria, ambazo, huhusu vita, vizazi, mashujaa, usuli wa kitu au jambo Fulani. Nne, kuna kigezo cha muktadha wa utendaji wa ngano. Katika kigezo hiki, kinachoangaliwa ni ngano inatendwa wakati gani na kwa mazingira gani. Kwa mfano,kwa kutumia kigezo hiki tunaweza kupata ngano ambazo zinatendwa wakati wa mbalamwezi, ngano zinazotendwa wakati wa ibada, ngano zinazotendwa wakati wa mapumziko ya wawindaji wakati wa kazi.

Hivyo kwa kupitia vigezo hivi, Okpewho aliainisha aina tatu za hadithi. Aina hizo ni ngano fafanuzi. Hizic dni aina ya ngano ambazo hufafanua asili ya kitu au wazo kwa kuzinagatia mazingira na tajriba ya jamii. Kwa mfano, ngano zinazoelezea asili ya kuumbwa kwa ulimwengu na nagano zinazosawiri sifa na tabia za viumbe katika mazingira yao. Aina ya pili hujumuisha visasili na visaviini. Kundi hili, hujumuisha hadithi zinazohusu wanyama, viongozi wa dini iwe katika ulimwengu au vyenginevyo. Uainishaji wa ngano, bado unautatanishi kwani kigezo kimoja, huweza kujitokeza zaidi ya mara moja katika aina nyengine za hadithi. Hivyo, mgawanyo wa hadithi umekuwa na

mitazamo tafauti. kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa (1988), wameelezea aina mbali mbali za hadithi za kimapokeo. Aina hizo ni kama hizi zifuatazo:

### 2.2.5 Ngano

Ngano ni hadithi za paukwa pakawa … wakaishi raha mustarehe. Wakati mwengine zimonyimbo. Kwa kawaida ni hadithi za maadili ambazo husimuliwa katika mazingira ya starehe, nazo huadili kwa kutumia istiara, kharafa na hekaya. Huwana wahusika wadudu, wanyama, binaadamu, mizimu na hata miungu, aidha ni viumbe visivyo na uhai kama; mawe na miamba. Wahusika hawa hupewa urazini, wa binaadamu ili kuadilisha nao huwa ni bapa.

### 2.2.6 Tarihi

Tarihi ni hadithi ambazo husimuliwa juu ya matukio ya kihistoria. Matukio hayo huweza kuwa ni ya kweli, ila hufumwa katika sanaa yenye ubunifu ndani yake, kwa kadri ya kuupeleka ukweli katika masafa fulani kutoka kwenye sanaa. Mara nyingi wahusika wake ni binaadamu, ila hawa hupewa uwezo mkubwa au mdogo mno kuyakinisha matokeo yanayozungumziwa na kuyawekea mantiki. Hadithi hizo mara nyingi, huongelea historia za wafalme, koo za utawala, kuanza kwa kabila, ukoo na kadhalika. Kwa mfano kumbukumbu za kuzaliwa kwa watu, kama zilivyojitokeza katika Qur-ani. Kumbukumbu za hadithi fupi zinazohusu matokeo maalumu kama vile mabaa, magonjwa, maafa, vita na njaa. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili, kuna hadithi kama ile inayoeleza chanzo cha chura kuwa na mabaka na jongoo kuwa na mwili mororo unaomeremeta. Huelezwa kuwa wote wawili walikwenda kwa sungura ili kuomba ushauri wapendeze. Wakati sungura anawashauri, chura alikuwa anadakiza kwa pupa. Hatimae churaalimuuliza sungura “Tukisha chemsha mafuta ya nyonyoo tujitumbukize ndani?” Kwa kuwa sungura alikuwa amebughudhiwa sana akamjibu “ndio”. Basi chura akaenda akachemsha mafuta na kujitumbukiza. Matokeo yake alipata ngozi

isiyopendeza. Jongoo aliyetuliya na kumsikiliza sungura vizuri na kufuata maelezo na akawa na muili mororo.

### 2.2.7 Visasili

Visasili ni hadithi ambazo, pamoja na kuwa na wahusika wa aina tafauti ambao pia ni bapa, hasa miungu na binaadamu, husimulia juu ya matokeo ya maumbile na ya kawida. Hadithi hizo hujaribu kueleza, juu ya imani na dini za jamii. Aghlabu hadithi za aina hiyo hutambwa mivigani.Visasili, hutumia mitiririko sahili na wahusika bapa. Kwa upande wa hadithi za kihistoria yaweza kuwa tafauti kidogo ingawa si aghalabu.

### 2.2.8 Vigano

Vigano ni hadithi fupi fupi zinazotakiwa kutumiwa kama mifano. Zina wadhifa wa methali. Zinakuwa ni picha na kutokana na picha hizo kunakuwa na uhawilishaji wa maana. Kigano ni kiishara aina ya kitaswira chenye mapana kuliko methali,kinachotakiwa kuhawilishwa ili kitowe maana. Kwa Kawaida kigano kinajengwa juu ya kituko kimoja tu, nacho hutumiwa kueleza kitukocha aina hiyo hiyo kiishara au katika maisha halisi. Wanaendelea kueleza kuwa aghalabu, vigano hupotea kutokana na kufungamana na miktadha na kuzuka kutokana na mazungumzo.

### 2.2.9 Soga

Soga ni hadithi ndogo ndogo zinazoelezea utani na aghlabu hadithi hizo huwa na ucheshi. Hadithi za aina hiyo hutolewa katika mtiririko wa matukio yenyekuleta uchekeshaji. Soga hujengwa juu ya tukio moja tu ambalo hukusudiwa kuchekesha. Katika kufafanua zaidi juu ya dhana ya soga, Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa wake wametowa mfano wa soga, unaotokana na utani, miongoni mwa Wapare na Wachaga:

Mchagga, Mhindi na Mhaya walipatana kuzikana. Kwanza alikufa Mhindi, kwa hiyo ilibidi wamzike. Mhaya akatoa fungu lake la shilingi elfu tano.Mchagga akatoa mchango

wake wahundi ya shilingi elfu kumi. Mchagga akachukuwa mchango ule, wa mhaya na akatoa hundi yake ya elfu kumi. Mhaya alipouliza kwa nini? Alijibiwa “ndugu yetu atabadilisha hiyo hundi huko mbinguni”.

Maelezo hayo ya mgawanyo wa aina hizo za hadithi kama yalivyotolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa ( washatajwa ) yamesaidia sana katika kutujengea uelewa juu ya aina za hadithi hizo za watoto ambazo tulizifanyia uchambuzi. Mgawanyo huo ambao kwa kiasi kikubwa umeangalia dhamira za hadithi, uliweza kutusaidia kwa kutupa muelekeo wa namna ya kuzipata dhamira ambazo zimejitokeza katika hadithi mbali mbali tulizozifanyia uchunguzi.

## 2.3 Dhana ya Dhamira

Kwa mujibu wa Sengo (2009), dhamira ni sehemu ya maudhui, na maudhui ni yale yasemwayo na maandishi ya kazi ya fasihi. Sengo (ameshatajwa), anaeleza kuwa dhamira ya mtunzi wa asili yaweza kuwa, ni mgogoro wa wanandoa, maandishi yakatoa dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe, viongozi wa juu wa serikali, kutokusikilizana kwa vilabu vya mpira, skuli na skuli na kadhalika. Baina ya neon naneno, katikati, ndani na nje ya maneno, mishororo, huwa mwapatikana visa na mikasa ya ajabu.

Sengo (ameshatajwa), aghlabu, muhusika mkuu, hubeba dhamira kuu msemaji mkuu ni mwakilishi wamtunzi. Kuna kazi ambazo humpa nafsi, huyo mtu aitwe “mpumbavu” kusema sema ya kipumbavu, kumbe hayo ndiyo kweli aliyoikusudia mbunifu ama yale yanayodhihirisha na ubunifu wenyewe.

Maelezo hayo ya Sengo juu ya dhana ya dhamira, yametupa uelewa mkubwa juu ya kuweza kuchambua dhamira za katika hadithi za watoto. Maelezo hayo yalikuwa yamepiga hatua kubwa na ya kina zaidi, juu ya dhana ya dhamira. Maelezo hayo

yametuongoza jinsi ya kuangalia vipengele, kama vile, vya wahusika, lugha iliyotumika na miktadha, ambayo yote kwa pamoja, yalitusaidia katika kufanya utafiti wetu huu. Hivyo kuweza kupata dhamira mbali mbali katika hadithi ambazo tumezifanyia utafiti.

## 2.4 Uchambuzi wa Vipengele vya Fani

Katika Kazi ya fasihi, kuna vipengele vya fani, ambavyo husaidia kuibuwa dhamira kama vilivyojadiliwa na hamad na wenzake (1981) kama hivi ifuatavyo

### 2.4.1 Wahusika

Huwa watu, aghalabu, na pengine huwa, wanyama “kama shamba la wanyama hadithi ya George Orwell, ambao wanaiongozahadithi katika muundo wa mazungumzo na migogoro ni ya wanyama. Pia wahusika wanaweza kuwa ni watu au viumbe vyengine vyovyote. Wahusika mara nyingi katika kazi ya fasihi ndio wanaobebesha migogoro ambayo ndiyo inayotoa dhamira ya kazi za fasihi. Muhusika mkuu katika kazi ya fasihi ndie anayebeba dhamira kuu.Kwani yeye ndie kiwakilishi cha mtunzi.

### 2.4.2 Mazingira

Njogu na Chimerah (1998), Hali inayozungumza hadithi katika tendo au mahala, shamba au mjini-kisiwani au bara, Afrika au Ulaya. Mandhari ni kipengele kimojawapo ambacho katika kazi ya kifasihi husaidia kuibuwa dhamira. Inategemea muundo wa mandhari ulivyojengwa na muhusuka katika kisa anachokisimulia. Mandhari inaweza kuwa ya kidhahania, kama vile mbinguni, ujinini nakadhalika au mahali halisi kama vile baharini, mtoni, nyumbani, jukwaani nakadhalika. Mandhari ya kazi ya fasihi inaweza kuibua dhamira kwa kuhusishwa na wahusuka na mtendo yao. Kwa mfano, iwapo kazi ya fasihi imemchora muhusika aliyetembea masafa marefu msituni kwenye vitisho na mazimwi, kwa lengo la kwenda kazini, basi mandhari hiyo inaweza kuibuwa dhamira ya umuhimu wa kufanya kazi.

### 2.4.3 Lugha

Huwa ni lugha ya nathari yenyehisiya ikilinganishwa na ile ya ushairi na ambayo hukamatana pia na ishara,sitiari na tamathali nyingi za usemi.Katika mtiririko wa lugha kuna mtindo wa simulizi,mtindo wa kurejelea  pengine pamoja na mazungumzo. Katika kazi ya fasihi lugha mara nyingi ndio inayotumika kufikisha ujumbe kwa jamii. Lakini ili kazi ya fasihi iwe na mvuto, msanii hutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile sitiri , methali, tashbiha, tauria, takiriri, tanakali sauti nakadhalika. Vipengele hivyo iwapo vitapangiliwa vizuri vinaweza kusaidia kuibuwa dhamira katika kazi ya fasihi. Kwa mfano, takriri katika kazi ya kifasihi huonsha msisitizo juu ya jambo Fulani linalohusika.Kwa hivyo mhakiki wa kazihiyo anaweza kuibuwa dhamira kutokana na takriri hiyo, ambayo pia itaweza kutowa ujumbe kwa jamii husika.

## 2.5 Baadhi ya Vipengele vya Maudhui

### 2.5.1 Ujumbe**ni**

Maazimio yanayotolewa kutokana na dhamira. Katika kazi ya kifasihi lazima kutakuwa na dhamira zinazohusika katika kazi husika, kutokana na dhamira hizo mhakiki wa kazi ya kifasihi anawza kuibuwa ujumbe ulioupata kutoka katika dhamira aliyoiibuwa na kuichambuwa. Kwa mfano ujumbe uliopatikana katika tasnifu hii umetokana na dhamira zilizoibuliwa na kuchambuliwa. Kwa mfano dhamira ya “ukaidi” imetupa ujumbe wao,” watoto kila wanalotaka kulifanya ni vyema washirikiane na wazazi wake.”

## 2.6 Utalii wa Kazi Tangulizi

Senkiwa (1974), amekusanya hadithi tisa za kienyeji. Madhumuni ya kukusanya hadithi hizo ni kudumisha utamaduni, elimu, na maarifa ya babu zetu, yaani mawazo yao, kuhusu maisha. Katika hadithi hizo, ameonesha matumizi ya lugha jinsi yalivyowapa wanafunzi nafasi ya kuielewa n a kuipenda lugha yao. Katika kazi hii, mtafiti amepata mwanga kwa kuikamilisha kazi yake ya utafiti kwani nahau na methali zilizotumika zilimsaidia katika uchambuzi na uibuwaji wa dhamira.

Wafula na Njogu (2007), wameeleza kuhusu nadharia ya muundo huku wakirejelea kwa Leech na Short (1981), ambao wana maoni ya kwamba, fasihiniumbo lenye viungo viwili, maudhui na fani na kwa hivyo viungo hivyo vinaweza kutenganishwa. Hapa muundo unalinganishwa na mtindo.

Wanaeleza pia kuwa muundo huvikusanya pamoja vipengele vya lugha na kuvipa umbo moja lisiloweza kugawika kwani viungo hivyo, haviwezi kuleta maana kwa kila kimoja kikiwa peke yake. Kazi hiyo imetusaidia sana, katika kuangaliya miundo ya hadithi tulizozikusanya, pia imesongesha mbele katika kutuelekeza kuhusu nadharia tutakayoitumia inayobainisha lugha.

Maghanga (1984), katika utafiti wake, alichambua ngano tano na alishughulikia maudhui kwa kutumia nadharia ya kimarx. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu uchambuzi wa baadhi ya vipengele vya kimaudhui vilivyochambuliwa katika tasnifu hiyo ndio msingi wa fasihi yoyote ile, ambapo hata katika tasnifu yetu hii tumejadili baadhi ya vipengele vya maudhui, vikijumuisha dhamira na ujumbe.

Njue (1989), amechambuwa ngano za Kiswahili akiangalia ujumbe pamoja na mafunzo kwa jamii ilizozisimulia. Pia, alishughulikia ploti ya ngano na umuhimu wa fasihi kwa jumla. Utafiti wake ulizama zaidi katika ujumbe na mafunzo, ambayo niSteer (1889), alizikusanya hadithi simulizi kutoka kwa jamii za Waswahili wa Zanzibar na kuzihariri. Lengo la Steer (keshatajwa) lilikuwa ni kuwahamasisha watu wengine waliojua kusoma na kuandika, kupata picha ya uandishi wa hadithi za Kiswahili, ambazo miongoni mwao, ziliburudisha, zilifunza, zilionya, ziliadilisha, kurithisha amali njema na tamaduni za jamii. Kazi hiyo ya Steer (keshatajwa) ilituelekeza jinsi ya kuzihariri hadithi tulizozikusanya katika jamii ya Wapemba. Vipengele vya msingi katika tasnifu hii na

itatuongoza kuona jinsi vipengele hivyo vya kimaudhui vilivyochambuliwa ili na sisi tuige kulingana na hadithi tulizoziteuwa na uhailsia wake ulivyo.

Timammy (1990), katika tasnifu yake ya uzamili alihakiki fani katika hadithi za jamii ya Waswahili. Amechambuwa matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Utafiti wake umetowa msukumo mkubwa katika kazi hii hasa katika vipengele vya fani ambavyo mara nyingi ndivyo vinavyoibua dhamira katika kazi ya fasihi. Uchambuzi wake ulimsaidia mtafiti wa kazi hii, kuvidurusu vyema vipengele vya fani.

Njogu na Chimerah (1999), wamezungunzia fani katika ngano kwa upana, na wakasema kuwa fasihi haiwezi kutenganishwa na vipengele mahsusi kama vile methali, jazanda, tashbiha, chuku, tanakali sauti. Mjadala wao kuhusu tamathali hizo za usemi, umekuwa na manufaa kwa utafiti wetu kwa sababu uchambuzi wao wa fani umetuwekea muhimili mzuri wakuchambua dhamira za hadithi za watoto na hasa pale walipoelezea simulizi na wahusika katika utafiti huo.ani na kumsaidia kukamilisha tasnifu yake.

Wamitila (2003), amejadili vipengele vya fani. Vipengele, alivyovishughulikia ni msuko, kusimuliya na tamathali za usemi. Pia, ametuonyesha, ngano ambazo tayari ameshazihariri.Kazi yake imetupa msukumo wa kuzihakiki hadithi za watoto kwa lugha za kitamathali zilizotumika, kwa kuibua dhamira zahadithi teule tulizozishughulikia katika utafiti wetu na kwa hivyo tumepata mwigo wa kuvichambuwa vipengele vya fani vilivyojitokeza katika hadithi teule zilzokusanywa katika jamii ya Wapemba.

Said (2005), aliangalia mafunzo ya ngano katika jamii ya Wazanzibari. Kutokana na utalii huo mtafiti ameona ipo haja ya makusudi ya kuchunguza dhamira za hadithi za watoto zinazopatikana katika jamii ya Wapemba, kwa vile, kazi nyingi tangulizi zilionekana kutoandikia utanzu huu wa hadithi katika jamii ya Wapemba na mtafiti

alihofia, utanzu huo ukasahaulika ikawa hasara kubwa kwa watoto na vijana wengi kisiwani Pemba.

Ngolena Henero (2006), wamefanya utafiti wa ngano katika jamii ya Wasukuma nchini Tanzania. Wao walichambuwa na kufafanua zaidi matumizi ya methali katika hadithi hizo. Kwa vile mtafiti alikuwa anaangalia baadhi ya vipengele vya lugha uchambuzi wa methali huo ulimuwezesha mtafiti kuangalia matumizi ya lugha yalivyochambuliwa na kumpa mwongozo katika kazi yake, hasa kwa kuwa katika utafiti wetu tumeangalia lugha ilivyotumika katika hadithi mbalimbali tulizoziteuwa kutoka katika jamii ya Wapemba.

Haji na wenzake (2007), walionesha mafunzo ya hadithi, mafunzo hayo ni kama vile; "kufikiria vizuri, lile tunaloomba na isiwe tunaomba kwa maneno ya hovyo, kwa kuwa hatujui, dua ni wakati gani itapokelewa"."Ikiwa mtu atakuwa ameshikilia kikweli, Dini ya Mwenyezi Mungu si aghalabu mtu huyo kufikwa na matatizo ya kidunia". Kwa hivyo tasnifu hii imetusogeza mbele katika kuijadili na kuonesha dhamira zilizopatikana katika hadithi teule zilizomo katika jamii ya Wapemba.

M'Nganithi (2008), anajadili vipengele vya fani, isitoshe amezungumzia kuhusu mtindo na maudhui, ploti, wahusika, usimulizi, mandhari, dhamira na aina toafauti za ngano, kazi yake imetusaidia katika kujadili vipengile vya maudhui katika ngano teule za Kipemba.

Nchimbi (2008), ameonekana kuzungumzia tanzu za fasihi na ameonesha dhima za fasihi katika jamii.Vile vile alifafanua uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui. Nchimbi (ameshatajwa) amevichambua vipengele vya maudhui na vile vya fani katika kuhakiki kazi za fasihi, mfano alituonesha matumizi ya lugha katika kazi za fasihi na akasema lugha ya kifasihi ni lugha ya kisanaa.

Dosha (2010) aliangalia mchango wa hadithi katika kuendeleza mila na dasturi za Waha, katika Kata ya Muluhona, wilaya ya Kasulu. Lengo alilotilia mkazo ni kutumia fasihi simulizi, kuifahamu kazi ya kisanaa ya jamii ya Waha, kwa lengo la kuimarisha sanaa hiyo ili iende na wakati. Katika hadithi alizozikusanya, aliibua maudhui na mafunzo ya kiuchumi pamoja na hali za maisha katikavipengele vya kifani kama vile muundo na mandhari. Mwandishi alikusanya hadithi kama vile kisa cha mume na mke, kisa cha mama wa kambo, asie sikia la mkuu, wajinga ndio waliwao na shibe mwana malevya. Kwa hivyo utafiti huo unaonekana kutoa mchango mkubwa kwa utafiti tulioufanya ambao unahusu kuchambuwa dhamira zinazopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba na hasa kwa vile hadithi hizo za watoto huwa na mfanano wa baadhi ya vipengele kama vile muundo na mtindo. Kwa mfano, mara nyingi, huwa na mtindo wa kutumika kwa nafsi zote tatu yaani nafsi ya kwanza, ya pili na hata ya tatu. Lakini pia hadithi hizi mara nyingi huwa na muundo wa moja kwa moja, hasa ukizingatia kwama, utafiti wetu, uliangalia baadhi ya vipengele vya fani, vikiwamo muundo na mtindo wa hadithi teule.

Nyamsende (2012), utafiti wake unahusu usawiri wa taswira za wahusika wanyama katika ngano za Waikizu. Hadithi alizozikusanya, zinaonekana na ujumbe, kama vile ushauri mbaya, usitegemee bahati ya mwenzio, tenda wema uondoke, usiache mbachao kwa msala upitao, ukubwa wa pua si wingi wa makamasi. Pia, alionesha uchambuzi wa taswira za wahusika wanyama katika ngano teule, dhima na nafasi ya taswira za wahusika wanyama.

Kwa hivyo utafitiwa Nyamsende (keshatajwa), umetoa msaada mkubwa katika utafiti tulioufanya ambao umeangalia dhamira za hadithi za watoto, kwani katika utafiti wakekumeoneshwa vipengele vya kifani na kimaudhui, ambavyo kwa kiasi fulani,

vimetuongoza katika utafiti huu hasa wakati wa kuchambua dhamira katika hadithi tulizozichagua kutoka katika jamii ya Wapemba.

Mapunda (2012) aliangaaalia hadithi zilizosimuliwa kwa lugha ya Kinyiha.Mapunda (kehatajwa) alieleza dhamira zilizopatikana katika hadithi hizo za kabila la Wanyiha ambazo zimefasiriwakwa lugha ya Kiswahili na akagunduwa dhamira, falsafa, mwelekeo na ujumbe. Dhamira alizogundua ni kama vile: Dhamira ya ukombozi, kuacha uchoyo, uzuri wa kufanya kazi na, ubaya wa tamaa. Vile vile, alichambuwa vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na mandhari. Kwa kutalii kazi hiyo mtafiti amepata mwanga mzuri katika utafiti wake alioufanya juu ya dhamira zinazopatikana katika hadithi za watoto.

Omar (2013), alijadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema katika skuli za upili visiwani Zanzibar.Alitafiti na kuainisha shida alizozipata mwanafunzi anayefundishwa maadili visiwani Zanzibar. Vilevile, alitafiti mbinu mpya za kufundisha hadithi simulizi katika kufunza maadili visiwani ambazo zingewawezesha Wazanzibari wengi kujifunza hadithi simulizi kwa urahisi. Tasnifu hiyo ilituongoza vyema katika kutuonesha jinsi ya kuzichambuwa hadithi.

Silau (2013), alifanya utafiti unaotoa tathmini kuhusu dhima ya nyimbo, katika kukuza nakuimarisha malezi.Akitoa mifano yake katika kabila la Wakaguru. Aliangalia dhima za nyimbo za kabila hilo, na vipengele vya fani katika nyimbo hizo, kama matumizi ya lugha na vyeginevyo. Katika kuiangalia kazi ya Silau (kashatajwa) mtafiti alipata muongozo mzuri wa kazi yake. Kwa kuwa nay eye pia aliangalia vipengele vya fani, yakiwemo matumizi ya lugha yaliyojitokeza katika hadithi alizozikusanya.

## 2.7 Mwega wa Nadharia

### 2.7.1 Maana ya Nadharia

Kwa mujibu wa Sengo (2009), nadharia ni wazo kuu,fikra kuu, muongozo mkuu wa mtu au watu(jamii)wa pahala fulani, wakati fulani,kwa sababu fulani. Nadharia ya utafiti ni muongozo wa kufuata wakati wa kuchambua kazi za kifasihi, kuonesha maelekezoya kufuata katika vitendo vya utafiti. Kwa maelezo hayo ya Sengo(ameshatajwa), tunaweza kusema, nadhahria nitaarifa au kikundi cha taarifa zilizoanzishwa kwa sababu za msingi, zinazotetea ukweli fulani wa jambo linalo kusudiwa kuelezea ukweli fulani au tukio fulani. Jambo hilo litawasaidia kuelewasentensi fupi juu ya matumizi ya nadharia. Mtafi katika uchambuzi wa data zake alitumia nadharia kama vile nadharia ya simiotiki, mwitiko wa msomaji, nadharia ya kijamii (sosholojia).

### 2.7.2 Sababu za Kuchaguwa Nadharia Hizo

Sababu ya kuzichaguwa nadharia ya simiotiki ni kupata kuchambuwa fumbo na fumbuzi zilizomo katika hadithi za watoto.Nadharia ya ujamii (sosholojia) ilitumika ili mtafiti apate fursa ya kuhusisha muktadha wa hadithi na maisha ya kila siku katika jamii ambamo hadithi hizo zinatambwa.Vile vile nadharia ya muitiko wa msomaji imetumika ili kutoa tafsiri kutokana na ufahamu wa mtafiti mwenyewe na sio kukokotwa na mawazo ya watu wengine waliofanya kazi kama hizi.

### 2.7.3 Nadharia ya Kijamii

Kiini cha nadharia ya kijamii ni tabu kidogo kuzibainisha,ila mijadala kadhaa hurejelea kwa Ugiriki ya kale.

Wafula R. na Njogu K. (2007), wanasema muasisi wa nadharia hii ni Herington na iliasisiwa katika mwaka wa2005,anaelezea etiemolojia ya nadharia ya kijamii.Nadharia inajikita katika misingi mikuu kama vile familia,elimu,dini,urasimu na utabaka.Hata

hivyo katika kila jamii mambo haya yamo. Kila mojawapo ya misingi hiyo, hushughulikiwa kwa kina katika msingi wa familia. Nadharia hii inachunguza jinsi tafauti zinavyojitokeza kati ya familia na familia na tafauti za jamii hadi jamii.Tafauti hizo zinahusu elimu, ndoa,malezi, imani za kidini,kanuni na miiko ya kijamii.Nadharia ya kijamii itamsaidia mtafiti kupata fursa ya kuhusisha muktadha wa hadithi na maisha ya kila siku katika jamii ambamo hadithi hizo zilitambwa.

### 2.7.4 Nadharia ya Simiotoki

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara, Fednad De Souse katika miaka ya1970, katika matumizi ya lugha kuna vitu viwili, kuna kitaja na kitajwa, na mara nyingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kitajwa, ndio maana kitu kimoja kinaweza kuitwa majina tafauti katoka jamii mbili tafauti. Nadharia hii inatufahamisha matumizi ya lugha ya ishara yanarejelea nini.

Nadharia ya simiotiki ina matawi matano, ambayo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihemetiki, msimbo wa kiurejelezi, msimbo wa kiseme na msimbo wa kiumaduni. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia msimbo wa kiurejelezi. Msimbo huu hutumia mneno yenye kurejelea mambo mbalimbali ambayoyana uhusiano fulani na maneno yenyewe. Nadharia hii ilimsaidi mtafiti kuchambuwa lugha za ishara zilizotumika katika hadithi teule zilizokusanywa katika jamii ya Wapemba.

### 2.7.5 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Kwa mujibu wa Wafula R. na Njogu K. (2007), nadharia ya muitiko wa msomaji iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya1960-1970, waasisi hawa ni Wajerumani, wanaamini kuwa kazi ya fasihi, inapaswa kutazamwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake, na si kutokana na uzoefu wa mwandishi.

Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira, kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja, bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Kwa hivyo mtafiti aliitumia nadharia hiyo ilikutowa tafsiri kutokana na ufahamu wake mwenyewe kulingana na muktadha wa hadithi iliyosimuliwa.

## 2.8 Hitimishoa

Katika sura ya pili mtafiti alishudhulikia utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Dhana mbalimbali zihusuzo mada zilizungumzwa. Kama vile dhana ya hadithi, fasili ya ngano, dhana ya fasihi ya watoto na dhana ya dhamira. Aina mbalimbali za hadithi zilionyeshwa katika sura hii. Mfano ngano, tarihi, visasili, vigano na soga. Baadhi ya vipengele vya kifani na kimaudhui vilizungumzwa, na kuangaliwa watangulizi mbalimbali ambao mtafiti aliwapitia ili kumuonesha mwanga, kujua watafiti wengine walifanya nini na yeye kazi zao zitamsaidia vipi katika utafiti wake. Mtafiti pia katika sura hii alizungumzia mwega wa nadharia. Nadharia tatu alizielezea, ikiwa ni pamoja na nadharia ya kijamii, simiotiki na nadharia ya mwitiko wa msomaji.

# SURA YA TATU

## 3.0 MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inahusu vipengele kadha ikiwemo sababu za kuchaguwa mbinu teule ambayo nimbinu ya mahojino, ikaonesha faida na hasara za mahojiano, uteuzi wa watafitiwa, jedweli la watafitiwa. Muundo wa utafiti ulielezwa.

### 3.2 Maana ya Mahojiano

Kwa mujibu wa Mulokozi (hana mwaka), mbinu ya ushuhudiaji maskanini inaweza kuwa ni pamoja na mahojiano, na alisema mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu au ya kidijitali au barua pepe kati ya watu wawili au zaidi kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa.Mtafiti aliitumia mbinu ya maktabani ili imsaidie katika kujua ni maeneo gani ambayo yameshaandikiwa ili nae mtafiti ajuwe atambae maeneo yepi ili asije akarudia kilichokwisha kuandikiwa. Na mbinu ya mahojiano ilitumika katika kukusanya data maskanini kwa watafitiwa.

#### 3.2.1 Sababu za Kuchagua Mbinu ya Mahojiano

Mtafiti alichagua mbinu ya mahojiano kutokanana maumbile ya mada yake. Mbinu hii ilimuwezesha kukutana na watafitiwa ana kwa ana katika mazingira yao halisi wanayoishi, ambayo mtafiti aliyahaulisha katika hadithi alizosimuliwa huku akiakisi dhamira zilizoibuliwa katika hadithi teule alizosimuliwa**.**

#### 3.2.2 Faida za Mahojiano

Kwa mujibu wa Mulokozi (1983), wameeleza faida na hasara za njia ya mahojiano kama hivi ifuatavyo: Hukuruhusu kuuliza maswali ya papo kwa papo na kufahamiana na mhojiwa, mfano yeye ni nani na ana maoni gani. Pia hukusanya tafsiri za wahusika kuhusu matukio yanayotafitiwa. Mtafitiwa anaweza kutowa ufafanuzi zaidi juu ya data

anazozitowa iwapo kuna maneno ambayo mtafitihaelewimaanayake. Mahojiano piahuwaruhusu wahojiwa kueleza misukumo nasababu za mienendo yao, kitu ambacho kitamsaidia mtafiti wakati wa uchambuzi wa data iwapo itahusiana na utafiti wake. Kutokana na faida hizo mtafiti aliweza kukusanya data kwa urahisi, na kuzichambuwa kwa ufanisi kwani aliweza kupata ufafanuzi wa moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa wake, katika vipengele mbalimbali vinavyohusiana na data alizozikusanya.

### 3.2.3 Hasara za Njia ya Mahojiano

Wahojiwa wengine hushindwa kujieleza kutokana na haya au sababu nyengine. Wapo baadhi ya watu hawana mazowea ya kuingililiana na watu wasiowajuwa, kwa hivyo huweza kujisikia shida kutoa maelezo juu ya lile mtafiti alilomuuliza.Kutokana na baadhi ya wahusika kutokujuwa umuhimu wa utafiti wanaweza kukupa ahadi zisizokuwa za kweli, kitu ambacho kinaweza kuchelewesha upatikanaji wa data kwa wakati.Pamoja na kasoro hizo, mtafiti aliweza kukusanya data vizuri, kwani alijitahidi kuwaelimisha watafitiwa wake juu ya umuhimu wa kile alichotaka kukifanya. Na aliwatowa hofukwa kuwaahidi kuwa data atakazozikusanya zitabakia kuwa ni siri.

### 3.2.4 Uteuzi wa Watafitiwa

Mtafiti alitumia mbinu ya bahati na sibu katika kuwapata walengwa katika vijiji teule. Alichaguwa uteuzi wa aina hii kwa sababu mbinu hii inaondowa upendeleo. Walengwa wote walikuwa ni kumi na tano, kila kijiji watu watano na walikuwa katika mpango huo uliopo hapo chini katika jedweli.

### 3.2.5 Jedweli la Watafitiwa

| *KIJIJI* | *WAZEE* | *WATOTO* | *WME WAZEE NA WATOTO* | *WAKE WAZEE NA WATOTO* |
|---|---|---|---|---|
| MICHENZANI | 3 | 2 | 2 | 3 |
| MKANYAGENI | 3 | 2 | 2 | 3 |
| SHIDI | 3 | 2 | 2 | 3 |

Jumla ya wazee wote waliohojiwa ni 9.Wazee hawa mtafiti aliwapata kwa njia ya unasibu, njia ambayo ilimuwezesha mtafiti kufika katika eneo la utafiti, na kubisha hodi nyumba yoyote. Alipokaribishwa ndani, mtafitiwa alijitambulisha na akaanza mahojiano na watafitiwa iwapo katika nyumba hiyo alikutana na kundi lengwa la watafitiwa anaowahitaji kwa lengo la kukusanya data. Wazee walikuwa watatu kutoka kila kijiji. Mtafiti aliweka idadi hiyoili kupata uwiyano sawa wa vijiji teule. Jumla ya watoto wote waliohojiwa ni 6.Wawili kutoka kila kijiji, idadi na ujinsia ulizingatiwa ili kutowa uwiyano sawa wa kiidadi na kijinsia kutoka vijiji teule.

Watafitiwa walioteuliwa ni kumi na tano. Mtafiti alichaguwa idadi ya watafitiwa kumi na tano ili kutaka kupata idadi sawa ya watafitiwa walioteuliwa kutoka kila kijiji bila ya upendeleo.

### 3.3 Muundo waUtafiti

Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu humuwezesha mtafiti kukusanya data na kuzichambuwa kwa kutumia maelezo wa kimaelezo ambapo tarakimu huwa hazitumiki. Hivyo data katika utafiti huu zimekusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo, ingawa na tarakmu zimetumika kwa kiwango kidogo ili kuiweka wazi zaidi tasnifu yetu.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alijishughulisha na mbinu za utafiti. Alielezea mbinu ya mahojiano, akaelezea sababu za kuchagua mbinu ya mahojiano, faida na hasara za mahojiano. Mtafiti alikusanya data zakekwa kutumia mbinu hiyo.Mbinu za uteuzi wa watafitiwa zilionyeshwa jinsi mtafiti alivyozitumia katika utafiti wake. Pia muundo wa utafiti ulielezwa kitu ambacho kilisaidia katika kuweka bayana uchambuzi wa data zilizokusanywa.

# SURA YA NNE

# 4.0 UCHAMBUZI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inahusu uchambuzi wa data, imeangalia dhamira zilizojitokeza katika hadithi za watoto za jamii ya Wapemba. Dhamira kama vile ukaidi, ujasiri, malezi, ushujaa, uongozi mbaya, kusaidiana, uchoyo, kibri, dhamira ya kazi, subira dhamira ya makaazi, ubinafsi, urafiki, ujanja, ubadhirifu wa mali, nafasi ya mwanamke, ukarimu, dhamira ya uzembe, uvunjaji wa sheria, utawala bora, unyonyaji, umoja na msikamano, kutoa maonyo, mapenzi na ndoa na uhalifu. Pia sura imeonesha, ujumbe uliopatikana katika hadithi teule za Kipemba, na baadhi ya vipegele vya fani vilivyosaidia kuibuwa dhamira katika hadithi za watoto za Wapemba. Vipengele hivyo niwahusika, matumizi ya lugha, muundo mtindo na mandhari.

## 4.2 Uchambuzi wa Data

Data zimechambuliwa kwa kuuzingatia dhamira zinazopatikana katika hadithi simulizi za watoto katika kisiwa cha Pemba.Uchambuzi wa data umefuwata hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwanza kuzisoma hadithi zote, pili kuchambuwa dhamira katika hadithi wanazotambiwa watoto pamoja na ujumbe unaopatikana katika hadithi hizo, pia tulivichambua baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira katika hadithi teule.

## 4.3 Dhamira Zilizopatikana Katika Hadithi Zilizokusanywa Katika Jamii ya Wapemba.

### 4.3.1 Dhamira ya Ukaidi

Ukaidi ni tabia ambayo anakuwa nayo mtu, na anakuwa hakubaliani na wazo au jambo lolote hata kama hana sababu za msingi, ingawa kama jambo hilo linaweza kuleta

madhara kwake au kwa mtu mwengine iwapo anaendekezwa. Katika hadithi ya kwanza, dhamira hii ya ukaidi imethibitishwa kuwapo katika jamii ya Wapemba. Hata hivyo,kwa kiasi fulani tabia hiyo inaonekana kukemewa kupitia dhamira za hadithi hiyo.Hii ni kutokana na kawaida ya fasihi simulizi kuionya jamii kwa lile lisilokubalika katika jamii husika.

Dhamira ya ukaidi katika hadithi ya kwanza ya Zimwi imethibitikakupitia muhusika Pate, pale aliposhauriwa na wazazi wake asikubali kuolewa na mtu wasiemjuwa tabia wala nasabu yake. Kutegemeana na nadharia ya kijamii ambayo hushughulikia kwa kina msingi wa familia, na tafauti zinazohusu elimu, ndoa, malezi, imani za kidini, kanuni na miiko ya jamii. Hii ndiyo sababu jamii yoyote ya ulimwenguni lazima ijikite katika vipengele hiviili kulinda mila na desturi za jamii hizo. Kwa hivyo wazazi wa Pate nao walikataa mtoto wao kuolewa na mtu wasiemjuwa kwa sababu huo ndio utamaduni wa jamii yao, kuwa wanandoa ni lazima wawe wanajuilikana na wazazi wa pande zote.

Pate yalimkuta yaliyomkuta kutokana na ukaidi na kuvunja miiko ya jamii yake.Nahuo ndio uhalisia ulivyo. Kwa hivyo hadithi inaitaka jamii ya Wapemba, hasa watoto wasipende kuvunja miiko ya jamii na familia zao.

### 4.3.2 Dhamira ya Ujasiri

Ujasiri ni hali ambayo mtu anafanya maamuzi bila ya woga tena kwa kujiamini na kuwa na msimamo usioyumba. Katika jamii ya Wapemba watu wanaojiamini, inaonekana wapo, pia jamii inahimizana kuwa na tabia ya ujasiri, kwani mtu anapokuwa na ujasiri inaonekana anaweza kuepukana na matatizo. Mfano katika hadithi ya kwanza, muhusika Pateanaonekana kuwa na ujasiri wa hali ya juu kwa kuweza kumtoroka mume wake bila ya kurudi nyuma wala kuwa na hofu ya aina yoyote. Hakujali watu wengine watamsema kwa kiasi gani, juu ya maamuzi aliyochukuwa ya kumtoroka mume wake.Mtafiti

anaonekana kutoa uchambuzi huu kwa kuongozwa na nadharia ya muitiko wa msomaji, iliyompa msomaji uhuru wa kutowa fasiri kulingana na maoni yake jinsi alivyofahamu alichokifafanuwa.

### 4.3.3 Dhamira ya Malezi

Malezi ni tabia ya wazazi kukaa pamoja na watoto wao, wakawapa huduma zote za msingi na kuwaongoza katika tabia njema huku wakizingatia mila na dasturi katika jamii zao. Kwa mfano, katika hadithi ya kwanza, wazazi wa Pate wanaonekana kulitilia maanani suala la malezi kwa kuwalea watoto wao hadi wakakuwa, na kufikia kupata mume. Pate kabla ya kuolewa, alikuwa chini ya uwangalizi wa wazazi wake, kwa maana hiyo ni wazi kuwa malezi katika jamii ya Wapemba, ni kitu kinachoangaliwa kwa umakini mkubwa, na malezi yao yanaonekana yanajali zaidi mtoto kuishi na wazazi wake nyumba moja na sio mtoto kuishi katika nyumba yake peke yake. Kwa hivyo kwa mtazamo wa mtafiti anaona mtoto hutakiwa awe na kwao. Uchambuzi huu umefanywa na mtafiti kwa kuongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji inayompa uhuru msoaji kuihakiki kazi ya fasihi kutokana na ufahamu wake. Pia nadharia ya kijamii imemuongoza mtafiti katika uchambuzi wake, kwani inaangalia mienendo ya familia na kuzingatia mila na desturi za familia na jamii husika.

### 4.3.4 Dhamira ya Ushujaa

Ushujaa ni hali ya kutenda jambo kubwa linawashinda watu wengi, au mtu kufikwa na jambo na akaweza kulivumilia ili aweze kulipatia utatuzi na wakati huohuo anawakinga wengine wasipatwe na athari. Dhamira ya ushujaa imejitokeza katika hadithi ya kwanza kupitia muhusika Miza pale alipomuona shemegi yake akiwa na tabia na vitendo visivyo vya kawaida (zimwi) na akawa hakuogopa hadi pale alipomshuhudisha dada yake, pia ushujaa huohuo, waliuonesha Miza na dada yake Pate, walipokimbia na kurudi kwao

bila ya kusita au kuwa na hofu fulani, na huu ndio ahalisia ulivyo mtu akipatwa na tatizo mara nyingi hutafuta njia yoyote ili ajikwamue na aondokane na tatizo hilo. Mtafiti amefafanuwa hivyo kutokana na ufahamu wake kama nadharia ya mwitiko wa msomaji inayomuangalia msomaji na uzowefu alionao katika kutafsiri matini ya kazi za fasihi.

### 4.3.5 Dhamira ya Uongozi Mbaya

Uongozi mbaya ni uongozi ambao haujali maslahi ya wanaongozwa.Mara nyingi, kiongozi mbaya huwa na tabia zisizoendana na jamii anayoiongoza. Kiongozi huyo anakuwa hakubaliki katika jamii yake na wakati mwengine hata katika jamii nyengine. Katka hadithi ya kwanza dhamira hii ya uongozi mbaya imesadifu kupitia mume wa Pate. Mume wa Pate amezungumzwa kuwa ni zimwi. Zimwi kwa hapa imekuwa ni ishara kuwaelezea viongozi wabaya, ambao hupewa dhima fulani katika jamii lakini wakawa na tabia ambazo ni kinyume na hadhi walizopewa na jamii zao. Kupitia tabia hizo viongozi haohuzisambaratisha jamii zao kwa njia moja au nyegine, kwa mfano, Pate alipogundua kuwa mume wake ni zimwi aliona bora akimbie mapema kabla hajamdhuru, kwani zimwi ni mtu ambaye anaweza kufanya lolote kwa mtu mwengine, alimradi afanikiwe na lake.

### 4.3.6 Dhamira ya Kusaidiana

Kusaidiana ni kitendo cha kumtatulia mwenzako tatizo lililomkwaza. Katika hadithi ya kwanza dhamira hiyo imeoneshwa na muhusika Miza ambae alikubali kuchukuliwa na dada yake ili akamsaidie baadhi ya kazi nyumbani kwake.

Katika jamii ya wapemba suala la kusaidiana linaonekana kusisitizwa kupitia hadithi ya kwanza, linavyoonekana lina nafasi kubwa katika jamii ya Wapemba. Kitendo cha kusaidiana kwa Wapemba ni sehemu ya mila na desturi zao. Kwa hivyo kila mwanajamii atatakiwa kufuata muongozo huo. Kama inavyosema nadharia ya kijamii kuwa, kila jamii

ina miiko na utamaduni wake, kwa hivyo, jamii ya Wapemba na hata za maeneo mengine ya Tanzania suala la kusaidiana limepewa nafasi kubwa katika maisha ya kila siku ndani ya jamii.

### 4.3.7 Dhamira ya Uchoyo

Dhamira ya uchoyo imeelezwa katika hadithi ya pili, ya Chura na Jongoo. Ambayo inaonekana kuiasa jamii ya Wapemba kuachana na tabia ya uchoyo na hasa kwa jambo ambalo hawana elimu nalo. Kwa mfano hadithi imeonesha kuwa, katika jamii, kuna watu wenye uchoyo uliotawaliwa na pupa la kutaka kupata tu, bila ya kuzingatia uwezo wa lile wanalolipapia. Watu wenye tabia hiyo, mara nyingi hutegemewa kufikwa na majanga makubwa. Kutokana uwelewa mdogo wa lile wanalolifanya. Mfano Chura alionekana kuunguwa maji moto kutokana na pupa alilokuwa nalo kwa kupokea taaluma isiyokamilika. Mtafiti ameichambuwa dhamirahii kwa kuongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji, inayoeleza kuwa, msomaji ana uhuru wa kuihakiki kazi ya fasihi kutokana na ufahamu wake.

### 4.3.8 Dhamira ya Kiburi

Kiburi kimeoneshwa katika hadithi ya pili. Katika jamii ya Wapemba inaonekana kuna watu ambao wamejivisha ila hii ya kiburi, ambayo ni sifa ya Mwenyezi Mungu. Kazi ya fasihi siku zote haifanyiki tu, na kubuniwa kiholela bali huwa na lengo maalumu. Dhamira ya kiburi imehusishwa na mhusika Jongoo kwa hivyo, Jongoo ni ishara ya kuwakilisha wataalamu ambao wana tabia ya kuwafanyia kiburi wanaowahudumia, kwa kisingizio cha kuwa wahudumiwa hao wana mioyo mizito ya kufahamu au wanapupa la kutaka kupokea huduma harakaharaka, mfano, katika hadithi ya pili, chura, alifanyiwa kiburi wakati alipokuwa anaelimishwa jinsi ya kufanya ili na yeye ameremete.

Lakini kwa ghadhabu na kiburi alichokuwa nacho Jongoo, alishindwa kumpa elimu hiyo kikamilifu na mwisho wake, akamsababishia Chura maafa ambayo madhara yakeni ulemavu wa maisha. Ikiwa wataalamu watagoma kutoa elimu zao kwa wanafunzi ipasavyo, basi jamii ya Wapemba inaweza kupata athari kubwa, na kusababisha majanga makubwa katika jamii.

Kwa hiyo, kiburi katika jamii ya Wapembani muhali mkubwa ambao haukubaliki na unakemewa ili usije ukaigwa na vizazi vijavyo.

### 4.3.9 Dhamira ya Kufanya Kazi

Kazi ndiyo msingi wa maisha katika jamii zote. Katika jamii ya Wapemba, kulikuwa na azma ya makusudi ya watu kuhimizana kazi. Mfano huo unapatikana katika hadithi ya tatuna hadithi ya kumi na nne. Hadithi zimetuonesha dhamira hiyo ya kufanyakazi.Mfano, mhusika Makame wa Makame, ambaye alionekana kupenda kazi badala ya kukaa na kumtegemea mama yake tu kwa kila kitu. Hadithi imemuonesha Makame wa Makame, akiwa mwakilishi wa kutoa msisitizo katika jamii juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa vijana.Waachane na tabia ya kuchaguwa kazi kwa kutumia visingizio visivyokuwa vya msingi. Pia, hadithi hiyo imeonesha kuwa kazi ndiyo msingi wakujikombowa kwa tabaka la chini. Makamewa Makame alipoona maisha magumu, ndipo alipomwambia mama yake kuwa na yeye ni bora aungane na vijana wenzake akavue agoni (ni kambi ya wavuvi). Mtafiti ametowa uchambuzi huu kwa kuongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji uliomruhusu kuchambuwa matini kutokana na uwelewa wake juu ya matini aliyoisoma au kuisikiliza. Pia hadithi ya14, imetuonesha dhamira ya kuhimizana kazi. Mhusika Muhamedi, ambaye alikuwa anasuka vikapu na kumpa kibibi, akauze ili wapate pesa, ziwasaidie katika maisha yao ya kila siku. Kazi ndiyo njia pekee ya kujienguwa kutokana na adha zinazomkabili mwanadamu.

### 4.3.10 Dhamira ya Subira

Subira ni kitu cha msingi kwa binadamu. Katika harakati za maisha, binadamu anakutana na mambo mengi, yaliyo mazuri na mabaya, yanayofurahisha na yanayochukiza, na hayo yote, kama mtu hana subira, ni vigumu kupambana nayo. Subira ni sehemu mojawapo ya utu wa binadamu. Katika hadithi ya 3 na ya 13 dhamira ya ukosefu wa subira kwa baadhi ya wanajamii imeonekana katika jamii ya Wapemba. Ujumbe uliomo kwenye hadithiunawakanya wanajamii kuachana na tabia hiyo. Maendeleo yao yanaweza kurudi nyuma kwa kuvunjika moyo, pale ambapo, kasoro ndogo ndogo zinajitokezana wakashindwa kuvumilia. Kwa Mfano dhamira hii imedhihirishwa na mama yake, Makame wa Makame, pale mwanawe alipofariki, akashindwa kuvumilia na akalia hadi akapofuwa macho.

Katika jamii ya Wapemba, hadithi inawataka wanajamii kuwana subira, ili wasije kujisababishia matatizo pale watakapotahiniwa na Mwenyeezi Mungu kwa kupewa mitihani ya maafa.Pia hadithi ya 13 inatueleza kuwa, akina mama na akina baba wanatakiwa kuwa na subira, na hasa pale wanapokosa kizazi (watoto).Wasiseme maneno hovyo hovyo hadi wakafika kumkufuru Mwenyezi Mungu. Mtafiti alitowa uchambuzi huu kutokana na mawazo yake kwa kutumianadharia ya mwitiko wa msomaji inayoelekeza kwamba msomaji wa matini anaweza kuihakiki kazi ya fasihi kama anavyoifahamu yeye. Kwa hiyo waja wanatakiwa wasifanye kama alivyofanya mama yake Kijoka, kwa kuomba kuzaa tu japo kijoka, kitu ambacho Mungu alimtakabalia na akazaa kijoka alichokiomba.

### 4.3.11 Dhamira ya Makaazi

Dhamira hii inawiana na maisha ya kawaida. kwani watu wanakodi, wanajenga na wengine wananunua nyumba na wote hao lengo lao ni kupata makaazi ya kuishi na

familia zao. Hadithi ya 4, inatoa msisitizo wa watu katika jamii ya Wapemba, kujitafutia makaazi. Kwa kweli, maishaya mtu, hayakamiliki bila ya makaazi. Mfano, katika hadithi ya 4, paka alipomwambia panya, wajenge nyumba ili waweze kuwa na makaazi maalumu badala ya kutangatanga kila pahala.Na huu ndiyo uhalisia uliyomo katika maisha ya binadamu.

### 4.3.12 Dhamira ya Ubinafsi

Ubinafsi ni hali ambayo mtu hutaka kila kitu kiwe chake peke yake. Katika hadithi ya 4,dhamira ya ubinafsi imejitokeza. Dhamira hiyo imejitokeza pale panya, alipojenga nyumba na mwenzake paka, lakini baadaye akataka nyumba iwe yake peke yake, kwa kutumi ujanja.

Katika jamii ya Wapemba, wamo watu wenye ubinafsi. Hadithi ya 4, imeliibuwa tatizo hilo, ili kuitanabahisha jamii, kuachana na tabia hiyo ya ubinafsi, kwa vile ni tabia isiyokubalika katika jamii. Inaonekana watu wenye tabia ya ubinafsi, mara nyingi hufikwa na matatizo, mfano, katika hadithi ya 4, anaonekana panya, aliliwa na paka bila ya kutegemea kutokana na tabia ya ubinafsi iliyomtawala. Hali hiyo ilitokana na paka kupandwa na hasira, pale alipomuona rafiki yake aliyemuamini, kuishi naye sasa amekuwa na ubinafsi wa kutaka kumtowa katika nyumba yao ya ushirika ili aishi peke yake.

Na huu ndyio uhalisia wa baadhi ya watu wenye tabia kama za panya, wanapoona tayari maendeleo yamepatikana katika ushirika wao,hutaka kile kilichopatikana, kiwe chao peke yao, wanasahau kuwa mila na desturi za kibinadamu kufanya hivyo ni kukosea, kama inavyotueleza nadharia ya kijamii kuwa ili mtu aweze kuishi vizuri , lazima afuate utamaduni wa jamii anamoishi.

### 4.3.13 Dhamira ya Urafiki

Urafiki ni kitu cha kawaida katika jamii ya kipemba, Hadithi ya 4 inatuonesha urafiki wa paka na panya ulionekana wazi kwamba, si urafiki wa kweli, na hili ni jambo ambalo katika jamii ya Wapemba lipo. Hadithi ya 4, inatuonesha kuwa, katika jamii ya Wapemba, marafiki wanafiki wapo, pamoja na kwamba, wameishi pamoja, kwa muda mrefu na wanajuana vizuri na huku wakiwa wanaoneshana upendo kati yao. Mfano panya alikuwa wa mwanzo kuusaliti urafiki wake na paka, kwa sababu panya ndiye aliyeanza kutaka kumdhulumu paka mara tu, nyumba yao ya ushirika ilipokamilika.

Hivyo, hadithi inaikemea jamii ya Kipemba kuachana na tamaa za kutaka kujitajirisha kwa kutumia migongo ya wengine na kuvunja utu wao kwa marafiki zao. Mtafiti aliona dhamira hiyo aichambuwe kwa mtazamo huo, kama ilivyo elekeza nadharia ya mwitiko wa msomaji, inayosema kuwa msomaji wa kazi ya fasihi anao uhuru wa kuichambuwa matini ya kifasihi kutokana na ufahamu wake.

### 4.3.14 Dhamira ya Uchoyo

Uchoyo ni tabia ambayo katika jamii ya Wapemba, inaonekana kuwepo. Hadithi ya 4 na ya 8, dhamira ya uchoyo imesadifu. Mfano, hadithi ya 4, imetuonesha uchoyo wa panya dhidi ya paka, hii ni ishara tu inayowakilisha kundi la watu wanaojifanya kuwa, wao tu ndio wanaohitaji maendeleo,uchoyo wa aina hiyo huchukuliwa kama ni uchoyo wa uwadui, kwa kutaka kile kilicho cha ushirika akifanye kiwe chake peke yake. Watu wa aina hii katika jamii ya Wapemba huwa hawakubaliki, kama nadharia ya kijamii inavyotueleza, kuwa kila mwanajamii ili awe mtiifu ni lazima afuate kile ambacho jamii yake imemuamuru kufuata, ikiwa ni pamoja na kufuata utamaduni wa jamii husika.Kwa mfano, katika hadithi ya 4, panya anaonekana kuwa na uchoyo wa uwadui kwa kutaka kuifanya nyumba ya ushirika na paka iwe yake peke yake, kwa kutumia ujanja. Pia, katika hadithi ya 8, ya ukewenza, Bimaonevu, alikuwa na uchoyo wa kiuwadui, kwani

alisababisha kifo cha mke mwenziwe ili abakie kwa mume peke yake, na watoto wake tu. Vilevile, alikuwa akimtesa mtoto wake wa kambu, Makidi akawa hampi chakula cha kumtosha. Na mara nyingi huu ndiyo uhalisia wa baadhi ya mama wa kambu.

Kwa hivyo,kwa kupitia hadithi hizi ya 4, na ya 8 jamii inaaswa kuacha kujiingiza katika choyo.kisicho na manufaa kwao na kwa jamii zao. Katika jamii ya kipemba,kwa kiasi kikubwakuna uchoyo, unaonekana katika masuala ya kiuchumi, hasa katika mambo ya umilikaji wa mali, kama hadithi ya 4 ilivyomuonesha muhusika panya na paka katika suala la kumiliki nyumba waliyoijenga kwa ushirika lakini hatima yake panya akataka iwe yake peke yake.

### 4.3.15 Dhamira ya Ujanja

Ujanja unaonekana kutumika katika jamii nyingi za kitanzania,ikiwa kamanjia mojawapo ya watu kujiongezea kipato na kujilimbikizia mali, jambo ambalo si zuri. Kwa mfano, panya ni mwakilishi wa watu wenye ila hiyo, ya kujipatia mali kwa kutumia ujanja, mara zote hali hii inamuweka mtu pabaya asipate mafanikio kwa lolote. Ukweli ni kwamba, maendeleo yoyote katika jamii, hupatikana kwa njia ya uwajibikaji. Katika jamii ya Wapemba, hadithi ya 4, inawaonya wanajamii kuwa kusitokee kundi katika jamii, wakajifanya wajanja na wengine wakafanywa majuha. Wakasahau kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, ili waendelee kimaisha lazima washirikiane. Mtafiti ameichambuwa dhamira hii kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki, ambayo mara nyingi hutumika kufumbuwa fumbo ambazo zimetumika katika kazi za kifasihi, kwa mfano mtafiti ameweza kumrejelea Panya na kumfananiza na kundi la watu wenye tabia kama za Panya katika jamii ya Wapemba.

### 4.3.16 Dhamira ya Wizi naUbadhirifu wa Mali.

Katika jamii zetu za Kipemba, wizi na ubadhirifu wamali linachukuliwa kama ni tabia ya kawaida kusikika ikitendwa.Ingawa kiukweli ni suala la kuchukiza sana na kuombewa laana. Dhamira ya wizi na ubadhirifu wa mali imeibuka katika hadithi ya 5, kwa mhusika Sungura.

Sungura ni ishara ya watu ambao huwa wajanja na tabia ya wizi na ubadhirifu wa mali za watu. Sungura ni mnyama mjanja mwenye tabia ya wizi na uharibifu wa vitu shambani na majumbani. Jamii ya kipemba, inaaswa na hadithi hii ya tano, kuwa wanajamii wasiwe na sifa za Sungura kwani wakiwa na tabia ya wizi na ubadhirifu wa mali,maendeleo yao, yatarudi nyuma na wanaweza kuanguka kiuchumi, kisiasa na kijamii.

### 4.3.17 Nafasi ya Mwanamke

Katika jamii ya Kipemba, mwanamke wanatazamwakama ni mtu mwanye udhaifu mkubwa. Dhamira hii ya nafasi ya mwanamke imeoneshwa katika hadithi ya 3, 5, 6,7, 8, 12 na ya 13. Hadithi zote hizo zimemuangalia mwanamke kama ni mtu mzembe, mchoyo na mwenye mawazo mafupi katika kupambanuwa mambo. Mfano, hadithi ya 5, mke wa Nfaki alipoamini kirahisi, alipoambiwa na wanawe kuwa Sungura ndiye mgeni wao mualikwa, aliporudi mume wake alimgomba sana. Katika hadithi ya 8, Mwau alionekana ni mwanamke ambaye ni mwepesi kughilibika, kwani alikubali ushawishi aliopewa na shangazi yake na akavunja amri za mumewe, kitu ambacho kilisababisha kuvunjika kwa ndoa yake.

Pia, mwanamke amechorwa kama ni aduwi, mfano katika hadithi ya 8 ya wakewenza, Bimaonevu amesababisha kifo cha mke mweziwe na kumtesa mtoto wake wa kambu. Kwa hivyo, katika jamii ya Wapemba, inaonekana mwanamke bado anaendelea

kunyanyasika lakini pia wanawake wakorofi wapo. Hadithi zinaitaka jamii iache tabia hiyo na wakubaliane na dini yao ya kiislamu inavyowaongoza. Wapemba wote ni waisilamu na huo ndio ukhalisia wa maisha yao. Dini yao ni dini ya kweli naya pekee ya Allah kwa wote na vyote. Si klabu ya mpira ya kubadili katiba na kanuni. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji katika kuifafanua dhamira hii, kwani nadharia hiyo imempa uhuru mtafiti wa kufanya uchambuzi wa matini kutokana na ufahamu wake.

Katika jamii ya Kipemba, mwanamke anaonekana akili yake yachukuwa mambo kulingana na tukio au wakati kitu ambacho si cha kweli, bali mwanamke, kwa kiasi fulani, ni binadamu mwenye mawazo yanayobadilika, kulingana na wakati na matukio, kama inavyosemanadharia ya kijamii inayojikita katika kuangalia tafauto za kitabaka zilizomo katika jamii, ikiwa mojawapo ni hiyo hadhi ya mwanamke katika jamii ya Wapemba.

Kwa hivyo jamii ya wapemba, inamwanamke anayechukuliwa visivyo sahihi na hasa katika upande wa baadhi ya mila na dasturi zinazomtukuza mwanaume, bila ya kuangalia Uislamu umempa hadhi gani mwanamke katika jamii, tokea enzi na enzi za masahaba. Kwa hivyo, mwanamke amepewa uwezo wa urithi, kufanyakaziza kiuchumi, kama vile biashara, na hii ilithibitika kupitia Khadija mke wa Mtume Muhammad kwani alikuwa ni mfanyabiashara mzuri.

### 4.3.18 Dhamira ya Uzembe

Katika hadithi ya 5, dhamira ya uzembe imejitokeza. Jamii inatanabahishwa kulirekebisha tatizo hilo la uzembe, lisiwe na nafasi kubwa ndani ya jamii yao. Hadithi imeuonesha uzembe, kupitia mhusika Nfaki, bwana aliyefanya uzembe pale alipomkamata mwizi katika shamba lake na akawakabidhi watoto wadogo, kitu ambacho

kilimuwezesha mwizi kuwageukiya watoto na kuwapa maagizo kinyume na yale waliyoagizwa na baba yao.

Hadithi inatufahamisha kuwa katika jamii ya Wapemba, wapo watu ambao wana tabia ya uzembe, ambao wanatakiwa kuacha tabia hiyombaya, kwani uzembe ni jambo linaloweza kusababishahasara kubwa kwa jamii. Mfano uzembe wa Nfaki ulimrukhusu mwizi mzowefu sungura kutoroka, mwizi ambaye, kwa muda mrefu alikuwa anatafutwa na wanajamii ili wamkomeshe kwa tabia ya wizi na uharibifu wa mali. Dhamira hii mtafiti ameichambuwa kwakutumia nadharia ya kijamii, ambayo inaihimiza familia na jamii kijumla kufuata mila na desturi za jamii zao, ambazo siku zote huwa zinawataka wanajamii kutenda mema.

### 4.3.19 Dhamira ya Uvunjaji waSheria

Uvunjaji wa sheria ni kitendo ambacho kinaonekana kuwemo ndani ya jamii ya Wapemba. Katika hadithi ya 4, 5, 9 na 15, dhamira ya uvunjaji wa sheria imo. Kwa mfano, katika hadithi ya 5, mhusika Nfaki alimkamata mwizi, alishindwa kumpeleka kwenye vyombo vya sheria ili ahukumiwe, badala yake aliona bora ampeleke nyumbani kwake akamuhukumu mwenyewe anavyopenda kutokana na kosa alilolifanya mwizi huyo. Kwa hivyo, hadithi inaihimiza jamii ya Wapemba kufuata sheria katika kutafuta suluhu na hukumu. Katika jamii kusiwe na watu wakawa wako juu ya sheria bali watu wote, katika jamii, wawe wanaongozwa na sheria zao. Hadithi zinatuongoza kuwa ndani ya jamii ya Wapemba watu wanaovunja sheria hawakubaliki.Watu wanapokamatwa wakati wanafanya makosa ni vyema wapelekwe mahakamani. Mtafiti ameichambuwa dhamira hii, kwa kuongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji ambayo imemruhusu kutafsiri matini aliyoisoma au kuisikiliza kutokana na ufahamu wake juu ya matini husika.

### 4.3.20 Dhamira ya Unyonyaji

Unyonyaji ni kitendo cha mtu au watu kudhulumuwengine ili kujipatia kipato kutokana na jasho la wenzao. Dhamira ya unyonyaji imedhihirishwa na mhusika Sungura katika hadithi ya 5. Unyonyajikatika jamii ya Wapemba unaonekana kukemewa na kutokukubalika, Nfaki alimuandalia Sungura, adhabu ya kuchinjwa, adhabu aliyoiona ni muafaka kwa watu wenye tabia ya kujifanya makupe. Swali la unyonyaji katika jamii ya Wapemba linaonekana kuwepo.Mtafitiamechambuwa dhamira hii kulingana ufahamu wake, kwani hata nadharia ya mwitikowa msomaji inalikubali hilo la mtafiti kuchambuwa kazi ya fasihi kutokana na mawazo yake. Kwa hiyo jamii ya Wapemba inataka kusitokee watu wachache katika jamii wakawa hawawajibiki lakini wanajiingizia kipato kupitia jasho la wengine.

### 4.3.21 Dhamira ya Utawala Bora

Utawala bora katika kila jamii ni kitu ambacho kinahitajika. Katika hadithi ya 6, utawala bora unaonekana kuwa ni kitu cha msingi na unatekelezwa chini ya usimamizi wa mhusika Simba. Simba ni kiongozi ambaye alionekana kujali sana maendeleo ya jamii yake. Baada ya kuona kuwa katika kijiji chao, pana shida ya maji,yeyendiye aliwashauri raia wake wachimbe kisima ili waondokane na shida ya maji inayowakabili. Raia walikubali na simba nae akasimamia na huku akishiriki katika kazi pamoja na wanajamii.

Kwa hivyo simba ni ishara ya viongozi bora na wanaojali maslahi ya wanajamii ingawa ni mkali na mwenye kutisha. Hadithi inatufahamisha kuwa katika jamii ya Wapemba wapo viongozi wazuri ambao wanaongoza kwa kuzingatia taratibu za ubinadamu mwema. Nadharia ya simiotiki imetuongoza katika kuichambua dhamira hiyo ya utawala bora, ambayo humsaidia mtafiti kurejelea maneno yanayowiana na vitu fulani fulani.

#### 4.3.22 Dhamira ya Umoja na Mshikamano

Dhamira hii inapatikana katika hadthi ya 6 na ya13. Wahenga walisema, “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”. Dhamira hii ya umoja na mshikamano, inawakilishwa na wanakijiji katika hadithi ya 6, wanakijiji ambao, wanaonekana kupata mafanikio ya kimaendeleo, baada ya kushirikiana pamoja, katika kijiji kilichokuwa na watu wachache ambao walikuwa na nia mbaya dhidi ya maendeleo ya kijiji hicho. Fisi; mwakilishi wa watu wenye tabia mbaya, mara nyingi wapo katika jamii ya Wapemba ingawa, kundi hilo ni dogo sana lisiloungwa mkono na watu wengi katika jamii.

Hadithi ya 6, inatueleza kuwa, siku zote, “mkataa wengi mchawi”, hivyo hutegemewa kukutwa na matatizo mengi. Fisi alikuwa ni mkataa wengi, khatima yake, aliishia kuadhibiwa, kitu ambacho kilikuwa hakina sababu kama angekubali kuungana na wenzake katika kuchimba kisima cha wote ili waneemeke wote. Uchambuzi huo mtafiti aliufanya kwa kutumia nadharia ya kijamii inavyoitaka jamii kuishi kwa kuzingatia kanuni za jamii ambazo miongoni mwao ni wanajamii kuwa na umoja na mshikmano.

Katika hadithi ya 13 umoja na mshikamano, umeoneshwa na wahusika Ali na ndugu yake Juma. Bila ya kushirikiana Juma peke yake asingemuweza kumbeba samaki hadi nyumbani.Jamii inasisitizwa kuungana pamoja kifamilia na kijamii ili waweze kujiletea maendeleo.

#### 4.3.23 Dhamira ya Mapenzi na Ndoa

Katika jamii suala la mapenzi, huruma ya kina kirefuna ndoa, linaonekana kuhalisika. Utulivuwa maisha pale mwanamke na mwanamme wanapofikia umri wa kufunga ndoa, wafanye hivyo. Katika ndoa, kuna faida nyingi, moja ni ya kupata kizazi cha halali kitu ambacho ni sifa kubwa kwa mwanamke wa kiafrika, akiwemo wa Kipemba.

Dhamira ya mapenzi na ndoa, imeonekana katika hadithi ya 5, 7, 8, na13 Kwa mfano, katika hadithi ya 7, Mwau alipendana na Lau na wakafunga ndoa,wenyewewakawa wanaishi maisha mazuri katika nyumba yao yenye vyumba saba. Pia hadithi ya 13 imeonesha dhamira hiyo ya ndoa, Kijoka pamojana kasoro alizokuwa akionekana nazo nayeye alifunga ndoa nawalipendanasanana mke wake katika maisha yao.

Vilevile, katika hadithi ya 5, Nfaki alikuwa na mapenzi ya kweli na mke wake na waliishi vizuri hadi wakapata watoto. Kwa hivyo, hadithi inatuelimisha kuwa, katika jamii ya Wapemba, suala la ndoa limepewa umuhimu mkubwa na wazee, wako mstari wa mbele, katika kulisimamia hilo kwa watoto wao wanapofikia umri wa kuoa na kuolea. Na hiyo ndiyo haki yake ya msingi ya kimaumbile.Nadharia ya kijamii ilituongoza katika kufanya uchambuzi wa dhamira hii, ambayo miongoni mwa majukumu yake ni kushughulikia masuala ya kindoa katika jamii husika kulingana na mila na dasturi zao.

#### 4.3.24 Dhamira ya Uhalifu

Uhaliu katika jamii nyingi unafanyika. Katika kisiwa cha Pemba uhalifu unaonekana ni wa kiwango kidogo na unasababishwa na watoto kutokana na wazee wao kutokuwatendeya usawa katika malezi.

Hadithi ya 9, watoto walimuuwa Yamuimui kwa sababu ya kupendwa sana na watu wa mtaani. Pia hadithi ya 8, Muhamedi alichukuliwa na wenzake ili akauliwe kwa sababuwaliogunduwa kuwa mama yao anampenda sana kuliko wao. Mfano mwengine,ni katika hadithi ya 4, paka alimuuwa panya, kwa sababu ya kumtapeli kwa kumnyan’ganya nyumba waliyojenga kwa ushirika.

Kwa maana hiyo, hadithi hizo zinawazinduwa wazee na jamii ya Wapemba kuchukuwa tahadhari katika malezi hasa katika kipengele cha kumpenda mtoto. Jamii inatakiwa

kuachana na mambo ambayo yatasababisha kutokea kwa uhalifu. Watu wanapokoseana, wanatakiwa wasameheane, kama walivyofanya wanakijiji baada kugunduliwa kuwa Muhamedi, alitaka kuuliwa na ndugu zake, kwani watoto hawakuadhibiwa bali walikanywa tu, na wasifanye kama alivyofanya Paka kumuuwa Panya, kutokana na kosa alilolitenda. Mtafiti alitumia nadharia ya kijamii katika kuchambuwa dhamira hii ambayo inahimiza watu kuishi kwa kupendana katika jamii na huku wakifuata maadili ya jamii zao.

## 4.4 Ujumbe Uliopatikana Katika Hadithi Zilizokusanywa Katika Jamii ya Wapemba

Mosi, katika hadithi ya 1,ujumbe uliopatikana ni kuwaasa watoto, wawashauri wazazi wao kwa kila wanalolitaka kulifanya.Asiye sikia la mkuu, huvunjika guu. Huwasibu watoto na wakala hasara. Kwa mfano Pate, aliolewa na mume Zimwi, kwa ukaidi wake, hatima yake akakimbia kwa mume wake.

Pili**,** katika hadithi ya 1, tunaambiwa ukiona pahala au jambo la kimatatizo ni bora uondoke au uwachane nalo. Mfano,Pate alimkimbia mume wake, mara alipogunduwa kuwa ni zimwi pamoja na kuwa alimpenda sana.

Tatu**,** Katika hadithi ya 2, jamii inawataka walimu au wataalamu wa fani zote, wasiwe na ufidhuli, bali wawe na subira kwa wanafunzi. Watakapowafanyia ufedhuli, wanafunzi wataweza kuharibikiwa kutokana na wanafunzi hao kuikosa elimu wanayoihitaji kutoka kwa walimu hao. Mfano,jongoo alipofanya jeuri,akamsababishia mwanafunzi wake Chura kuunguwa maji ya moto, na akapata ulemavu wa ngozi wa maisha.Wanafunzi wanaposomeshwa wanatakiwa kupunguza pupa, na kumsikiliza vyema mwalimu, mfano, Chura alifanya pupa wakati wa kupewa mafunzo na mwalimu akakasirika.

Matokeo yake, Chura alikwenda kuifanyia kazi elimu isiyokamilika, akaunguwa kwa maji moto.

Nne, katika hadithi ya 3, tunapata ujumbe, kupende kufanya kazi, Makame wa Makame alikuwa ni kijana mpenda kazi, na hata umauti wake, ulimkuta akiwa katika kambi ya uvuvi ( agoni) ambako ndiko alikokuwa akifanya kazi ya uvuvi.
Tano, katika hadithi hii ya 3 tuapata ujumbe unaowashajihisha vijana na jamii kwa jumla kuwa, watoto ni vyema, kila wanalotaka kulifanya wawashauri wazazi wao ili kupata Baraka za wazazi wao. Kwa mfano, Makame wa Makame alipotaka kwenda agoni, kwa kuvua alimuomba mama yake, ruhusa na alipomrukhusu, ndipo akaenda.

Sita**,** katika hadithi ya 4 ujumbe unaopatikana ni kuwa, mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba, mfano panya kwa tamaa ya kumiliki nyumba peke yake, hatima yake alipoteza maisha na familia yake ikajenga uadui wa milele baina yao na paka.

Saba, hadithi ya 4, inatupa ujumbe usimuamini kila mtu,kwani huenda yule unaemuona ni mwema kwako, akawa ndiye aduwi mkubwa wako, mfano, Paka na Panya, walikuwa ni marafiki lakini baadaye Panya alikuwa wa mwanzo kutaka kumdhulumu rafiki yake Paka.

Nane, watu wasiwe na ubinafsi, kwani ubinafsi unaweza kumuweka mtu pabaya. Mfano, Panya aliyejenga nyumba, shirika na Paka, lakini kutokana na ubinafsi wa Panya akataka nyumba iwe yake peke yake. Kwa vile, yeye alikuwa ndiye fundi, aliitiya mlango, mdogoili paka asiingiye. Paka alizigunduwa njama zake na akaamuwa kumuua.

Tisa**,** hadithi ya 5, inatowa ujumbe kuwa wanajamii wasiwe wajanja katika kujiletea maendeleo na badala yake wawe ni wawajibikaji zaidi na hapo ndipo maendeleo

yatapatikana. Kwa mfano, katika hadithi, Sungura anaonekana kuwa mjanja na kutaka kujipatia kipato kwa jasho la wenzake, na siyo kwa nguvu zake, kitu ambacho kilimsababishia madhara.

Kumi**,** katika hadithi ya 5, ujumbe mwingine tunaoupata ni kuwa,ukiwa na rafiki yako, muwe na urafiki wa kweli.kwa mfano, Nfaki na rafiki yake aliyemualika ugeni, nyumbani kwake, kwa hivyo tabia kama hii ikiendelezwa katika jamii ya Wapemba inaonekana kuwa nzuri.

Kumi na moja**,** hadithi ya 5, pia inatupa ujumbe kuwa, ukikwepa sharia ujuwe utapatwa na matatizo. Mfano Nfaki alipomkamata mwizi shambani mwake alimpeleka kwake ili achijwe, lakini mwizi, alifanikiwa kutoroka.Kwa hivyo jamii ya Wapemba inatakiwa kufuata kanuni zaidi kuliko kuchukuwa hatua mikoni mwao.

Kumi na mbili**,** katika hadithi ya 6, ujumbe tulioupata ni kuwa, wengi wape, ukiona jambo linaungwa mkono na watu wengi, basi na wewe usilikatae, likubali hivyohivyo, kwani mawazo ya wengi mara nyingi huwa na faraja na wahenga walisema “hakuna ujinga wa watu wote”.

Kumi na tatu, hadithi ya saba inatupa ujumbe kuwa wanawake wafuwate amri za waume zao.na wasifuwate ushawishi wa watu wengine kwani wanaweza kuharibu ndowa zao, iwapo watatii amri za watu na kuacha amri za waume zao. Mfano Mwau aliachwa kwa sababu ya kufuata ushawishi aliopewa na shangazi yake na kuacha amri ya mumewe kwa kukifunguwa chumba cha saba alichoambiwa na mume wake asikifunguwe.

Kumi na nne**,** katika hadithi ya 8na ya 9, ujumbe tunaoupata ni wazazi kutokuwa na ubaguzi kwa watoto wao, na ikitokea mzazi kumpenda zaidi mtoto wake mmoja, basi

ajitahidi asiwadhihirishie wenzake, kuwa anampenda kuliko hao wenzake, kwani huwenda atamsababiahia matatizo. Kwa mfano, katika hadithi ya 9, Yamuimui aliuliwa na watoto wenzake, kwa sababu wazee wao, walikuwa wakimsifu sana Yamuimui, kwa uzuri wake, na wakawadharau watoto wengine, ambao Yamuimui kawazidi kwa uzuri. Pia katika hadithi ya 8, Muhamedi alitaka kuuliwa na watoto wenzake kwa sababu waligunduwa kuwa anapendwa sana na mama yao kuliko wao.

Kumi na tano, hadithi ya 12, inatowa ujumbe kwa vijana kwamba, wasichaguwe kazi, kwa sababu kazi ni kazi tu, alimradi iwe inaleta masilahi na inazingatia maadili mema ya jamii. Mfano Babu Dii alipoambiwa na kibibi, amrambe tongo ili aweze kupata pesa alikubali na akamramba, alimradi tu lengo lake lifikiwe.

Kumi na sita, katika hadithi ya 13,ujumbeni kuwa, tunapokuwa na shida zetu tusisememaneno mabaya. Inafaatuchaguwe ya kusema, kwani dua, wakatimwengine zinapokelewa haraka.Ukiomba dua mbaya utapata kibaya. Mfano mama wa Kijoka, kwa vile alikuwa hajapata mtoto, aliomba azae angalau Kijoka. Kwa hivyo, Mungu aliitakabali dua yake na akabeba mimba, alipojifuguwa kajifunguwa kilekile kijoka alichokiomba

## 4.5 Vipengele vya Fani Vilivyosaidia Kuibuwa Dhamira Katika Hadithi za Watoto Katika Jamii ya Wapemba

Vipengele vitakavyoangaliwa ni baadhi ya vipengele vya fani kama vile, wahusika,matumizi ya lugha na mandhari. Kwa upande wa wahusika tutaangalia wahusika wakuu tu. Tumechaguwa vipengele hivi kwa sababu mara nyingi,katika hadithi za paukwa ...........pakawa, kwa kiasi kikubwa ndivyo vipengele vinavyosaidia kuibuwa dhamira katika hadithi hizo.

### 4.5.1 Wahusika

Katika hadithi ya kwanza ya Zimwi kuna wahusika ambao wamesaidia katika kuibuwa dhamira tulizozipata,wahusika hao ni kama hawa wafuatao:

#### 4.5.1.1 Mhusika Pate.

Huyu ni muhusika ambaye amewakilisha kundi la watoto wa kike ambao wenye tabiya ya ukaidi katika masuala ya ndowa, hawapendi kuwasikiliza wazee wao, juu ya ushauri wanaopawa. Katika jamii ya Wapemba, baadhi ya watoto wanaonekana kuwa na tabia ya ukaidi. Hadithi inawakataza watoto kuachana na tabia hii na badala yake wasikilize ushauri wa wazee wao kwani wao ni watu wanaotumia hekima na busara katika kumuangalia mchumba wa kumuoza mwanawao kwa kuzingatia zaidi maadili aliyonayo mtu Muhusika huyu alisaidia katika kuibuwa dhamira ya ukaidi.

#### 4.5.1.2 Mhusika Mize

Mize ni mdogo wake Pate. Alimchukuwa kuishi naye ili amsaidie baadhi ya kazi. Mize ni mhusika anayewakilisha kundi la watoto wenye huruma na dada zao. Mize anaonekana kumsaidia dada yake kumpelekeya shemeji yake chakula shambani kila siku, pia Mize,alimnusuru dada yake, kuliwa na zimwi mara alipogunduwa kuwa shemeji yake ni Zimwi. Kwa hivyo, hadithi ya Mize, inaitaka jamii ya Wapemba kuwa, na utamaduni wa kusaidiana miongoni mwa wanajamii, pia kuepushana na matatizo kwa lile linalowezekana. Muhusika huyu alisaidia kuibuliwa kwa dhamira ya kusaidiana miongoni mwa hadithi zilizoteuliwa na kujadiliwa na mtafiti.

#### 4.5.1.3 Mhusika Mwengine ni Zimwi

Zimwi alikuwa mume wa Pate, Zimwi ni ishara ya watu ambao hawana tabia nzuri na hawakubaliki katika jamii ya Wapemba. Mhusika Zimwi, alikuwa akifanya uchawi wake kwa siri, wakati akiwa shambani ili mke wake na shemeji yake wasimuone. Hadithi

inaionya jamii ya Wapemba, kuachana na tabia mbaya ya kurogana ambayo haina manufaa yoyote kwa jamii. Kitendo cha Pate na mdogo wake, kulikimbia Zimwi ni ishara kuwa, Zimwi katika jamii ya Wapemba halikubaliki hata kama linakutunza kwa kiasi fulani na ana hadhi gani kwako, kwani Zimwi ni jitu lenye tabia mbaya lisilopendelea wenzake mema. Muhusika Zimwi alitowa mchango mkubwa katika kuibua dhamira ya uongozi mbaya.

### 4.6 Katika Hadithi ya 2ya Chura na Jingoo Kuna Wahusika Wafuatao

#### 4.6.1 Chura

Chura ni mnyama ambaye, mwendo wake ni wa kurukaruka kwa kutumia miguu yake. Chura ni ishara ya watoto ambao, huwa na pupa, katika kutenda mambo. Jamii inaaswa kuachana na tabia ya kurukia mambo, kabla hayajakamilika ipasavyo. Watoto wanatakiwa kuwa wapole na watulivu wakati wakifanya chochote, na hasa wanapopokeya mafunzo wanayopawa na walimu wao, wazee wao na hata wakubwa wao wengine. Uchambuzi wa dhamira hii, umeongozwa kwa nadharia ya simiotiki ambayo huyatumia maneno kiishara huku yakirejelea vitu vyengine. Kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii. Muhusuka chura alisaidia kuibua dhamira ya kiburi. Katika hadthi zilizoteuliwa.

#### 4.6.2 Jongoo

Jongoo ni mdudu ambaye, anapenda kuishi karibu na watu, ingawa watu hawampendi. Jongoo anaonekana kumeremeta mwili wake na anapendeza. Jongoo ni ishara ya watu ambao huwa na ukarimu mkubwa kwa watu, ingawa anaonekana kutawaliwa na kiburi na hiyo mara nyingi,ndiyo sifa ya watu wanaojiona kuwa kipaji fulani. Katika jamii ya Wapemba, watu wanatakiwa wasiwe na ufidhuli ili waweze kuwasaidia wale wanaohitaji msaada wao. Uchambuzi huo uliongozwa na nadharia ya simiotiki, ambayo inaamini kuwa katika kazi ya kifasihi kuna lugha za ishara, ambazo hurejelea vitu fulani

katika jamii husika. Muhusika huyu altowa mchango mkubwa katika kuibuwa dhamira ya kiburi.

### 4.7 Katika Hadithi ya 3 ya Makame wa Makame Kuna Wahusika Wafuatao

#### 4.7.1 Makame wa Makame

Huyo ni kijana ambaye anapenda kazi na wala hana tabia ya kuchaguwa kazi. ni kijana anayeweza kufanyakazi pahala popote. kwa mfano, Makame wa Makame, alikwenda kuvuwa na akahamia agoni hadi akafariki huko huko. Ni mhusika anayekubalika katika jamii ya Wapemba. Muhusuka huyu alifanikiwa kuibua dhamira ya kufanya kazi. Uchambuzi huu ulifanywa kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaiji, ambayo inaamini kuwa mtafiti anaweza kuitafsiri matini ya kifasihi kutokana na ufahamu wake.

### 4.8 Katika Hadithi ya 4 ya Paka na Panya Kuna Wahusika Wafuatao

#### 4.8.1 Panya

Ni mnyama ambaye ana ila ya uharibifu, na mwenye kukera sana watu katika nyumba zao. Panya ni ishara ya watu ambao wana tabia mbaya na wametawaliwa na ubinafsi wa kutaka kila kitu kiwe chake peke yake. Ni watu wanaopenda kuharibu mipango ya watu na maendeleo ya wenzao, watu wa aina hiyo hawakubaliki, katika jamii ya Wapemba na hawafai kuigwa. Mtafiti alifanya uchambuzi huu kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki, ambayo hurejelea vitajwa vinarejelea nini katika jamii. Muhusika Panya alisaidia kuibua dhamira ya uchoyo.

#### 4.8.2 Paka

Ni mnyama mwenye mahaba makubwa na watu. Anapenda kuwa karibu na watu. Maisha yake yako ndani ya majumba ya watu.Paka ana tabia nzuri na mara nyingi hufuata yale anayofundishwa na yule anayeishi naye. Paka ni ishara ya watu ambao mara nyingi, hushirikiana na wenzao kwa nia njema. Baadaye mema yao husalitiwa kwa

kudhulumiwa au kuonewa, kwa njia moja au nyingine, na hapo wema wao, na juhudi zao, husahaulika. Katika jamii ya Wapemba watu kama paka, wapo, ni watu ambao wanakubalika kwa tabia zao na wanafaa kuigwa katika jamii. Muhusika huyu aliibua dhamira ya subira.

### 4.9 Hadithi ya 5 ya Sungura ina Wahusika Wafuatao

#### 4.9.1 Nfaki

Ni mhusika, ambaye anonekana kupenda watu, na ni mkarimu sana. Alionekana kuwa na uzembe fulani. Alipomkamata mwizi shambani mwake, na akamkabidhi kwa watoto, wampeleke nyumbani kwake ili akamuadhibu. Hakumpeleka kwenye vyombo vya hukumu kitendo hicho kilimpa fursa mwizi kutoroka. Watu kama hao, katika jamii ya Wapemba, wapo. Muhusika Nfaki alifanikiwa kuibua dhamira ya uzembe. Uchambuzi huu uliongozwa kwa kutumia nadharia ya kijamii, ambayo inashughulikia maisha ya jamii na taratibu zao.

#### 4.9.2 Sungura

Kwa kawaida Sungura ni mnyama, ambaye ana tabia za ujanja na anpenda kufanya uharibifu kwa masilahi yake. Sungura ni ishara ya watu ambao wamo katika jamii ya Wapemba. Watu kama hao, wamo katika jamii zao, huchelewa kunaswa, wanaposhikwa, hutumia mbinu zote ili wakomboke dhidi ya makosa. Kwa mfano, Sungura, alipokamatwa na Nfaki, akimuharibia na kumuibia mazao yake, alijitahidi ili kutoroka aepukane na adhabu ya kuchinjwa aliyoandaliwa na Nfaki, na Sungura alifanikiwa kutoroka. Muhusika Sungura alisaidia kuibua dhamira ya ujanja, katika hadithi husika. Mtafiti alitoa uchambuzi huu kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki, ambayo kwa kawaida hufafanua lugha za ishara zilizotumika katika kazi ya fasihi.

### 4.10 Katika Hadithi ya 6 ya Fisi na Simba Tumewaona Wahusika Hawa Wafuatao:

#### 4.10.1 Simba

Simba ni mnyama mkubwa na mkali kuliko wanyama wote, mnyama huyu anogopewa na wanyama wote, na hakuna anayeweza kufanya jeuri mbele yake. Katika hadithi ya 6 simba ni ishara ya viongozi wakali lakini waliotawaliwa na busara, wanapokasirika huchukuwa maamuzi mabaya. Mfano Simba alimuahidi Fisi atakapo kuja akamkamata anachota maji katika kisima cha ushirika atamuadhibu vibaya na atajuta kwa alichokifanya. Katika jamii ya Wapemba viongozi kama hawa wapo. Viongozi kama hawa wanakubalika katika jamii na wanafaa kuigwa Muhsika Simba alifanikiwa kuibua dhamira ya utawala bora. Katika uchambuzi huu mtafiti alingozwa na nadharia ya simiotiki ambayo hurejelea tafsiri za lugha za ishara na kuhusisha hali halisi ya jamii.

#### 4.10.2 Fisi

Fisi ni mnyama mwenye tamaa kubwa. Katika hadithi Fisi ametajwa kama ni ishara ya watu wenye tamaa na kutaka kujilimbikizia mali kupitia migongo ya wenzao. Ni watu wasiopenda kujituma. Hadithi inatowa maonyo kwa watu hawa,wanatakiwa kuachana na tabia hii katika jamii zao, kwani maendeleo hupatikana kwa kujituma na siyo kwa kufanya ujanja. Muhusika huyu aliibuwa dhamira ya unyonyaji.

### 4.11 Katika Hadithi ya 7 ya Kungu Mauwa kuna Wahusika Wafuatao

#### 4.11.1 Mwau

Ni mwanamke ambaye aliolewa na akakabidhiwa nyumba ya mume wake aitunze pamoja na mali zote zilizomo ndani. Mwau alikuwa ni mke aliyekubali kushawishiwa ili avunje makubaliano aliyokubaliana na mume wake, alikubali ushawishi na akakifunguwa chumba alichoambiwa na mume wake asikifunguwe, kwa hivyo matokeo yake alisababisha kuvunjika kwa ndowa yake. Katika jamii ya Wapemba watu hawa wamo. Hadithi inaizinduwa jamii, na hasa wanawake, katika ndowa zao ni vyema waepukane

na vishawishi, kutoka nje kwani vinaweza kuwavunjia ndowa zao. Muhusika huyu aliibuwa dhamira ya nafasi ya mwanamke.

#### 4.11.2 Lau

Lau ni kijana ambaye alikuwa ni mrogaji, alikuwa na mke wake aliyeitwa Mwau, Lau alimpa mke wake talaka kwa sababu ya kulitorosha jini lake alilokuwa akilitumia kwa uchumi wa kila siku. Hadithi inatutanabahisha, katika jamii ya Wapemba watu kama Lau wapo, watu hao hawakubaliki na hawafai kuigwa. Muhusika huyu alisaidia kuibua dhamira ya wizi na ubadhirifu wa mali. Nadharia ya kijamii ndio iliyotumika katika uchambuzi huu. Kwani nadharia hii inajikita katika misingi inayoshughulikia mienendo ya jamii kama vile familia.

### 4.12 Hadithi ya 15 ya Muhamedi ina Wahusika Hawa:

#### 4.12.1 Muhamedi

Muhamedi ni mtoto aliyependwa sana na mama yake kuliko wenzake wengine, mhusika huyo ni kiwakilishi cha watoto wanaotokea kupendwa sana na wazazi wao hadi wenzao wakaona kero kutokana na kupendwa huko. Hatma ya watoto kama Muhamedi, katika familia zao, huweza kuchukiza kwa ndugu zao, na kusababishiwa maafa. Hadithi inasisitiza jamii kuwachana na tabia ya kuwabaguwa watoto. Muhusika huyu alisaidia kuibua dhamira ya malezi. Mtafitiwa alitumi nadharia ya mwitiko wa msomaji katika kuchambua muhusika huyo.

Pia Muhamedi alikuwa ni mtoto anaependa kujituma, alikuwa fundi mzuri wa vikapu ambavyo aliviuza na akawa anijiendeleza kimaisha yeye na bibi aliyemuokowa na kifo. Muhamedi ni mtoto anayekubalika kwa hivyo anafaa kuigwa.

### 4.13 Katika Hadithi ya 9 ya Yamuimui inaWahusika Hawa Wafuatao:

#### 4.13.1 Yamuimui

Ni mtoto mzuri kuliko watoto wote katika kijiji chao, pamoja na uzuri wake, watu wengi pale mtaani walimpenda,Yamuimui, alikuwa ni kero kubwa kwa watoto wenzake, hawakumpenda kwa sababu alisifiwa yeye na kutiwa kasoro wao. Hali hiyo ilimsababishia Yamuimui kifo, kwa choyo cha watoto wenzake. Hadithi inaionya jamii ya Kipemba kuacha tabiya ya kumpenda mtoto hadi wenzake wakajuwa kwani wanaweza kumsababishia matatizo. Muhusika huyu aliaidia kuibuwa dhamira ya mapenzi kwa watoto. Mtafiti alifanya uchambuzi huo kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaji, inayompa uhuru msomaji wa matini ya kifasihi kutowa ufafanuzi wa matini aliyoisoma kutokana na ufahamu wake.

### 4.13 Hadithi ya 12 ya Babu Dii Imetupatia Wahusika Hawa Wafuatao:

#### 4.13.1 Babu Dii.

Ninikijana anaependa kufanya kazi, anaejali kazi, bila kuchaguwa kazi, alimradi kazi hiyo italeta masilahi kwake au kwa jamii. Kwa kuyathibitisha hayo Babu Dii alitembea masafa marefu kutafuta kazi, na alipokutana na kibibi kizee kikamwambia amrambe tongo ndipo ampe kazi alikubali, kisha akamuajiri na maisha yake yakawa mazuri. Hadithi inaisisitiza jamii kupenda kujituma, na kuwataka vijana kuacha tabia ya kuchaguwa kazi, mradi iyendane na maadili yao. Muhusika huyu alitowa mchango katika kuibua dhamira ya kuacha kuchaguwa kazi. Ufafanuzi huo umetolewa kwa kutumia nadharia ya ya kijamii inayoshughulikia mienendo na tabia za jamii.

#### 4.13.2 Mke wa Babu Dii.

Ni mwanamke mwenye uvumilivu, kwa kumvumilia mume wake akenda kutafuta kazi na yeye akabakia nyumbani akiangalia familia, hadithi inatowa msisitizo kwa akina mama kuwa na subira za maisha kwa waume zao, wawe kama mwanamke huyo

wasiwatie wahaka waume zao wanapotoka kwenda kuhangaikia maisha (kutafuta kazi). Muhusika huyu aliibuwa dhamira ya nafasi ya mwanamke. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya muitiko wa msomaji. Ambayo imempa uhuru msomaji wa matini ya kifasihi kuhakiki kazi ya kifasihi kutokana na ufahamu wake.

### 4.13.1 Bibi Kizee.

Ni ishara ya matajiri wenye uwezo wa kuwaajiri watu, hawapendi wafanyakazi wazembe na wenye kuchaguwa kazi. Matajiri hawamuajiri mtu kwa cheti bali humuangalia umakini wake katika kazi.  Babu Dii alitakiwa arambe kibibi tongo hadi macho yafumbuke ndipo ampe kazi.  Watu kama hawa katika jamii ya Wapemba wanakubalika na wanafaa kuigwa. Muhusika Bikizee aliibuwa dhamira ya kutokuwa na uchoyo.

## 4.14 Katika Hadithi ya 13 ya Kijoka  Kuna Wahusika Hawa

### 4.14.1 Mama Yake Kijoka

Ni mwanamke ambaye alichelewa kupata watoto, anaonekana kukosa subira kwa sababu alipoona kakaa muda mrefu bila ya kupata mtoto, alikata tamaa na akaomba Mungu amjaalie azae japo kijoka. Hadithi inawataka watu katika jamii ya Wapemba  kuwa na subira juu ya mitihani yanayowakabili na wasishughulike,  wakakufuru kwa Mungu wao, kama alivyokufuru mama yake Kijoka na akazaa Kijoka. Muhusika huyu aliibua dhamira ya nafasi ya mwanamke, pia dhamira ya kutokuwa na subira. Nadharia ya kijamii ndiyo ilyotumika katika uchambuzi wa muhusika huyo. Kwani nadharia ya kijamii inaiangalia jamii katika vipengele vya familia, dini na mienendo mengine yote yanayohusu jamii.

### 1.14.2 Kijoka

Nyoka ni mdudu ambaye watu wengi wanamuogopa na hazoeleki kwa walio wengi. Kijoka ni ishara ya watu ambao huzaliwa na ulemavu, Kijoka alionekana kudharauliwa na watu  hasa alipokuwa akihitaji  huduma kutoka kwawanajamii, kwa mfano alipokuwa

akitaka mke kila mtu alisema hawezi kumuozesha mwanawe kijoka, akaja akamtafuna, kwa tabu alitokea mtoto mmoja akamwambia mimi nataka uniowe kwa sababu sisi tumasikini kwetu kwa hivyo bora mimi nichukuwe hizi pesa ili ziwasaidie wazazi wangu. Hadithi inaionya jamii ya Kipemba kuacha kuwanyanyapaa walemavu kwani nao ni watu kama watu wengine na wanahitaji kupata huduma zote za msingi.

### 4.15 Hadithi ya 14 ya mtu na ndugu yake wahusika Waliomo ni

#### 4.15.1 Binadamu

Ni rafiki mkubwa wa simba, alikuwa ni mtu asiekuwa na uvumilivu , kutokana na tabia ambazo simba alikuwa ndiyo maumbile yake, na hivi ndivyo walivyo binadamu, kutaka kila kitu kiwe kama wanavyopenda wao hata kama haiwezekani. Jamii ya Wapemba inatakiwa kubadilika,watu waishi kulingana na hali zao. Wasilazimishe mambo yasiyowezekana Muhsika huyu amesaidia kuibuwa dhamira ya kuwa na subira. Uchambuzi huu umefanywa kwa kuongozwa na nadharia ya muitiko wa msomaji.

#### 4.15.2 Simba

Ni mnyama mkubwa na mwenye nguvu, watu wanamuogopa, ana tabia ya kula watu. Katika hadithi simba ni ishara ya watu ambao pamoja na uwezo na mamlaka waliyonayo katika jamii lakini huwa na mahusiano mazuri na watu wa tabaka la chini, Simba alikuwa na urafiki mzuri na binadamu, Hadithi inaitaka jamii kuwa na tabia ya kuwathamini wale wasio na uwezo na hata kama unamuona mtu ni dhalili kiasi gani. Muhusika simba alisaidia kuibua dhamira ya utawala bora.

### 4.16 Hadithi ya 10 ya Bunuasi na Wafuatao

#### 4.16.1 Bunuwasi

Ni mtu anaejifanya mjanja, mwenye akili kuwashinda watu wote, anaonekana kutawaliwa na ubinafsi, alikuwa mwizi wa maji, usiku kisimani, na kuyachafuwa bila

ya kujali kuwa na wenzake watayahitaji, pia bunuwasi alikuwa muongo, kwa sababu alikataa kuwa maji aliyaharibu yeye, vilevile alimdanganya mgunya kuwa yeye kajificha ndani ya sanduku kwa sababu alikuwa akitaka kuozeshwa mtoto wa mfalme na yeye hamtaki, kitu ambacho siyo kweli. Bali, alitiwa sandukuni kwa lengo la kwenda kuadhibiwa. Katika hadithi mhusika huyu ametumika kama ni ishara ya watu wanaojifanya wajanja na wenye akili ili wawadhulumu wenzao. Katika jamii ya Wapemba wapo, na hawakubaliki.Muhusika Bunuwasi ni Muhsika aliyesaidia kuibua dhamira ya ujanja na ubinafsi.

Kwa hivyo hadithi imekusudia kuwazinduwa wanajamii kuwatambuwa watu wa aina hii ili wajuwe jinsi ya kuishi nao ili wasije wakawasababishi majanga miongoni mwao. Watu kama bunuwasi hawakubaliki katika jamii na wala hawafai kuigwa.

## 4.7 Matumizi ya Lugha Katika Hadithi Teule za Wapemba.

Kazi yoyote ya fasihi, haina budi kuangaliwa kipengele hichi cha lugha. Lugha ya kifasihi, hutumika ikiwa na lengo maalumu kwa hadhira yake. Lugha hiyo, hutimika, ikiwa ni kisaidizi katika kuibuwa dhamira na kufikisha ujumbe uliyokusudiwa kwa jamii.

Kimani na Chimera(1999), kwa mujibu wa mhakiki wa Kirusi, Roman Jacobson "Fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimakusudi", Roman anakusudia kusema kwamba, lugha inayotumika katika kazi ya fasihi, inavutia na kuwafanya hadhira kuifikiria kiundani. Kirumbi (1975), anasema kuwa "tunaposema lugha itumiwayo katika fasih, tunakusudiya kusema kuwa lugha hiyo imerembeshwa, ili ilete mvuto."

Wamitila (2003), anaeleza kuwa lugha ndiyo nyenzo inayotafautisha fasihi na sanaa nyengine kama uchoraji, ufinyanzi, ususi n. k.

### 4.7.1 Tamathali za Usemi

Wataalamu wametowa maana ya tamathali za usemi. Kuhega(1977), Wamiyila (2008), Mbatiah (2001) na Holman na Harmon (1986). Tamathali za semi ni dhanna ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa makusudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au ilyozoeleka. Tamathali ni nyingi sana lakini tutaangalia zifuatazo ambazo mara nyingi huweza kuonekana katika hadithi za paukwa .....pakawa.

**4.7.2 Tashbiha** hii ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye tabia tafauti. Msokile (1992), tashbiha hutumia ulinganishi wa "mfano wa", kama, mithili, sawa na ja. Msanii hutumia ulinganishi huu ili kujenga picha kwa hadhira. Kwa mfano, katika hadithi ya kwanza ya Zimwi kuna tashbiha hii, "Mkia ulikuwa unawaka moto mithili ya mwenge wa kurambazia madodo". Hadithi inaisisitiza jamii, ielewe kuwa, warogaji wako makini katika kukamilisha lengo lao la kuwaroga wenzao, jamii ya Wapemba inaaswa iachane na tabiya hiyo mbaya.

### 4.7.3 Tashhisi

Wales (2001), anasema, hii ni tamathali ya usemi ambayo, kitu kisicho na uhai, hupawa sifa za binadamu.Tamathali hii ya usemi hutumika ili kuleta mvuto wa lugha na athari za kihisia. Kwa mfano, "Jongoo kwa mapenzi alimjibu". "kaa humo shimo likule". Tashhisi hii ilisaidia kuibua dhamira ya kuwepo kwa kiburi, kwa wataalamu wa fani mbalimbali katika jamii ya Wapemba. Uchambuzi huo uliongozwa na nadharia ya simiotiki inayoshughlikia lugha za ishara zinarejelea nini katika kazi ya kifasihi.

### 4.7.4 Takriri

Msokile (1992), anaeleza takriri ni urudiyaji wa silabi, maneno, mistari na viungo vinavyofanana katika kazi ya sanaa. Lengo la kurudia maneno, huwa ni kutia msisitizo, juu ya jambo linaoelezwa. Kwa mfano, katika hadithi ya 13, tena toka! toka! mimi usinitafutie matatizo...., pia, hadithi ya 7, kuna takriri hii, " Mrudishe! Mrudishe!, maneno hayo alikuwa anaambiwa Mwau na mume wake, na katika hadithi ya 11 kuna takriri, "Wakenda, wakenda, wakenda weeee!, katika hadithi ya kwanza, "Muwamu weee! Muwamu weee! Maneno haya ilikuwa ni wito aliokua akiutumia Mize kumuita shemegi yake. Na shemegi yake ambae alikua Zimwi alimuitikia eeeeeee! ............... moto zima!Zima! nimuitikie muwamu. Takriri hii ilisaidia kuibua dhamira ya kuwepo kwa uongozi mbaya katika jamii ya Wapemba.

### 4.7.5 Tanakali Sauti

Wamitila (2003), anasema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambazo huigiza kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo n.k.Tanakali sauti huisaidiya hadhira, kupata picha ya lile linaloigiziwa hiyo sauti. Kwa mfano, katika hadithi ya Panya na Paka,..........panya akaanza kulia chwiii! chwiii!. Pia katika hadithi ya Chura na Jongoo, ipo tanakali sauti,............."chura akaondoka akenda nyumbani kwake kroo! kroo! kroo!"Takriri hizi zilisaidia katika kuweka wazi zaidi kwa baadhi ya dhamira kama vile dhamira ya ya kiburi, na dhamira ya uchoyo.

### 4.7.6 Taswira

Ni picha ambazo huijia hadhira akilini. Wanapoisoma au kuiangalia kazi ya fasihi, picha hizo huifanya hadhira kusisimka. Katika hadithi ya 12 ya Babu dii,"akamramba tongo bibi mpaka akawa anaona vizuri". Taswira hii imesaidia katika kutanabahisha juu ya umuhimu wa kuwa na kazi, na hali ngumu anayoipata mtu wakati anapotafuta kazi,.

Kwahivyo lugha hii ya kitaswira ilisaidia katika kuibua dhamira ya kuacha kuchagua kazi.

### 4.7.7 Methali

Hamad (1981), anasema, methali ni usemi mfupi wenye maana nzito au hekima ndani yake. Methali hutumialugha ya mkato, kuonya au kusisitiza jambo fulani, lugha huwa na mapigo maalumu ya kuleta ladha katika kazi ya fasihi. Aghalabu methali, hutumika katika kuadibu wadogo na kuwatanabahisha au kuwakumbusha wakubwa. Kwa mfano katika hadithi ya 13, kuna methali "mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe". Methali ilitumika ikiwa na na nia hilehile ya kuitanabahisha jamii juu ya mienendo yanayohusu mila na dasturi zao. Methali hii ilisaidia kuweka wazi dhamira ya malezi, kuwa ndugu wathaminiane, kwani huko ndiko kustiriana na kupendana.Mtafiti aliongozwa na nadharia ya kijmii. Ambayo imejikita zaidi katika katika familia, elimu, dini na mienendo mengine ya kijamii.

## 4.8 Mandhari

Njogu na Chimerah (1998), Mandhari ni mahali maalumu palipojengwa na mtunzi na mnamotokeya matukio ya kazi ya fasihi. Msanii hujenga mandhari yamsaidie kufikisha ujumbe alioukusudia kwa jamii. Hadithi zinaonekana na mandhari ya kijijini, kwani matendo ya wahusika yanaonekana kuhusika zaidi na ukulima, uvuvi na maendeleo madogo ikiwa ni pamoja na uhaba wa huduma muhimu, kama vile maji na elimu.

Katika hadithi ya 1, ya Makame wa Makame, mandhari iliyotumika ni ya kijijini kwani, wahusika wake wamevaa uhusika ambao ni wa kujishughulisha na kilimo na uvuvi, kwa mfano mume wa Pate anajishughulisha na kilimo cha kutwa, katika shamba lake. Mandhari haya yalisaidia kuibua dhamira ya kufanyakazi. Hadithi ya 12, ya Kijoka mandhari yake ni ya kijijini, mama wa Kijoka alikwenda msituni kutafuta kuni.

Mandhari hiyo ilisaidi kuibua dhamira ya kuacha unyonyaji, watu waijtume na wasiwe tegemezi. Hadithi ya 7, ya kungu mauwa, na imejengewa mandhari ya kijijini, kumetajwa miti mirefu na mito iliyoko msituni Mandhari hiyo ilisaidia kuibuwa dhamira ya umoja na mshikamano.kwani mito mirefu na miti iliyoka msituni ni ishara ya umoja. Vilevile katika hadithi ya 6, wanajamii kujadili kutatuwa shida ya maji waliyonayo,kitu ambacho, mara nyingi, huwapata watu wanaoishi vijijini. Mandhari ya hadithi teule yameundwa kijijini ili kusaidia kuibuwa dhamira na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kuifikia jamii ya Wapemba.

### 4.9 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alishughulikia uchambuzi wa data. Alichambua data kwa kuzingatia vipengele vitatu, ambavyo ni dhamira zilizopatikana katika hadithi za watoto za jamii ya Wapemba, ujumbe uliopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba na kuvibainisha baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira katika hadthi za watoto za jamii ya Wapemba. Katika kuchambua vipengele hivyo mtafiti aliongozwa na nadharia mbalimbali, ambazo alizitumia kama mwega katika kujenga hoja zake katika uchambuzi wa data zake.

# SURA YA TANO

# 5.0 HITIMISHI, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi wa Sura

Katika sura hii mtafiti alishughulikia,vipengele kama vile, hitimishi, muhtasari na mapenekezo.

## 5.2 Hitimishi

Lengo kuu la utafiti huu ilikuwa ni kuzikusanya hadithi za watoto katika jamii ya wapemba na kuchambuwa maudhui katika vipengele vya dhamira na jumbe vilivyojitokeza katika hadithi teule.Pia mtafiti alichambuwa baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibuwa dhamira katika hadithi za watoto za jamii ya Wapemba. Mtafiti amefanikiwa kuzionesha dhamira na kuzichambuwa, kama zilivyojitokeza, katika hadithi teule za jamii za Wapemba. Dhamira zilichambuliwa kwa kutumiya nadharia tatu, ambazo ni mwitiko wa msomaji, nadharia ya kijamii na nadharia yasimiotiki. Mtafiti alitumia nadhariya hizo kwa sababu ya maumbile ya kazi yenyewe ili zimsaidiye katika kuzichambuwa dhamira.

Ujumbe na baadhi ya vipengele vya fani vilivyosaidia kuibua dhamira. Inavyoonekana, lengo la utafiti lilifikiwa. Hii ni kutokana na kuziba pengo lililokuwepo, la kuvichambuavipengele vyakimaudhui kama vile dhamira na ujjumbe, vilevile kuvihambuwa vipengele vya fani vilivyosaidia kuibuwa dhaira katika hadithi teule za jamii ya Wapemba.Tasnifu hii imechambua zaidi dhamira za hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Lakini imechunguza katika vijiji vya Shidi, Michenzani na Mkanyageni tu, kwa hivyo, mtafiti mwengine yuko huru, kuchunguza katika vijiji vyengine na akaangalia fani katika hadithi hizo Katika vipengele vya muundo na mtindo.

## 5.3 Muhutasari wa Utafiti

### 5.3.1 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu , ambayo yaliongozwa na masuali matatu. Suala la kwanza lilikuwa ni, ni dhamira gani zilizopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba? Suala hili lilijibiw a kwa kuangalia dhamira zilizopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Dhamira kama vile, dhamira ya ukaididi, uzembe, makaazi, utawala bora, urafiki, uchoyo, ujanja, wizi na uharibifu wa mali, nafasi ya mwanamke, uvunjaji wa sheria, unyonyaji, umoja na mshikamano, mapenzi na ndoa, uhalifu, malezi , ujasiri na ushujaa.

Suala la pili lilikuwa, ni ujumbe gani uliopatikana katika hadithi za watoto katika maisha ya kila siku katika jamii ya Wapemba? Suala hili lilijibiwa kwa kuchambuwa ujumbe uliopatikana katika katika hadithi teule za jamii ya Wapembe. Ujumbe kama vile, watoto wawashauri wazazi wao kwa kila wanalotaka kulifanya, ukiona pahala pana jambo la kimatatizo ni bora uondoke au uachane nalo, walimu au wataalamu wasiwe na ufedhuli, kupenda kufanya kazi, mtaka nyingi nasaba hupata mwingi msiba, usimuamini kila mtu, watu wasiwe na ubinafsi, wanajamii wasiwe wajanja, muwe marafiki wa kweli, ukukwepa sheria ujuwe utafikwa na matatizo, wengi wape, wazazi wasiwe na ubaguzi na usichaguwe kazi.

Suala la tatu lilikuwa ni vipengele gani vya fani vilivyosaidia kuibuwa dhamira katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba? Suala hili lilijibiwa kwa kuvionyesha vipengele vya fani vilvyosaidia kkuibuwa dhamira katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Vipengele kama vile, wahusika, vipengele vya lugha na mandhari vilioneshwa na jinsi vilivyosaidia kuibuwa dhamira mbalimbali katika hadithi teule za jamii ya Wapemba.

## 5.4 Mapendekezo

Katika tasnifu hii mtafiti amechambuwa maudhui katika vipengele vya dhamira. Pia kuchambuwa ujumbe katika hadithi za watoto za paukwa pakawa zilizomo katika jamii ya Wapemba. Inavyoonekana ni kuwa hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba zimeanza kusahaulika, na hii huwenda ni kutokana na wakati wa sasa ulivyo, kwa wazazi na walezi kutingwa na shughuli nyingi za kimaisha na kukosa muda wa kukaa na watoto wakawasimulia hadithi kama ilivyokuwa hapo zamani. Kwa hivyo napendeza wazazi na wanajamii wa kipemba watenge muda maalumu wa kukaa na watoto wao ili wabadilishane nao mawazo kwa kuwafunza kupitia utanzu huu wa hadithi simulizi za watoto.

Wakati mtafiti alipokuwa akisoma kazi tangulizi alibaini kuwa utanzu huu wa hadithi simulizi ambao ni moja kati ya tanzu za fasihi, haujaandikiwa sana ukilinganisha na tanzu nyengine za fasihi kama tamthilia na ushairi. Kwa hivyo napendekeza watafiti wa kiswahili katika tawi la fasihi wachukuwe jitihada za makusudi, waandikie utanzu huu wa hadithi za watoto ili usije ukasahalika na kuja kuonekana ni kitu kisichokuwa na maana kwa vizazi vijavyo. Vyombo vya habari navyo ni vyema viwe na vipindi vya kuhamasisha juu ya umuhimu wa utanzu huu. Ikiwezekana waandae hate vipindi vinavyohusiana na hadithi simulizi za kijadi za watoto.

## MAREJELEO

Afrika Corporation (1977),*Ecyclopedia American volume 11* New YorkAmerican Corporation.

David, S. (1974*), Mazungumzo ya Babu Zetu,Kitabu cha Pili* Oxford University Pres Dar-es –salaam Nairobi.

Doshe, E. A. (2010), "Mchango wa Hadithi Katika Kuendeleza Mila na Desturi za Waha,"Tasinifu ya Uzamili, Dares-salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Fineganm, R. (1970) Oral Literature in Africa, London Oxford University.

Haji, A. I. (2007*), Fasihi Simulizi Zanzibar,*Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Zanzibar.

Halmen, C. na Harmon K. (1986*), Face of Islam in Africa Literature* London,Heinman Potsmouth.

Hussein, E. (1988)*, Kwenye Ukingo wa Thim*. East Africa Ltd. Nairobi.Oxford University Press.

Kirumbi, P. (1975)*Misingi ya FasihiSimulizi*, Nairobi Shungwaya Publisha Ltd.

Kothari, C.R.(2004), *Research Methodology,Methods and Techniques*,New Delhi,NewAge International.

Kuhenga, C. (1977), *Tamathali za Usemi*, Dar es salaam. East Africa Literature Burean

M'ngaruthi, M.(1980), *Fasihi Simulizi na Utamaduni* Nairobi Jomo Kenyata Foundetion.

Maghanga, J. (1984) "Fasihi simulizi katika jamii, uhakika na ngano za kidawida". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mapunda E. B. (2012), "Project ya osw 324",Dares alaam:Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Materu, L. M. (1989) "*Utafiti, mbinu na ukusanyaji wa fasihi simulizi na hatima yake*".

Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya Fasihi* Nairobi Standard Text Books,Graphics and Publishing .

Msokile , M. (1992*), Misingi ya Hadithi Fupifupi*, Dar es salaam: University Press.

Msokile , M. (1993*), Misingi ya Uhakiki wa Fasihi* Nairobi. Jomo Kenyata Foundetion.

Mulokozi, M. M. (1996), Fasihi ya KiswahiliDaresalaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Nchimbi, A. S. (2008), *OFC 008 Kiswahili,* Dares Salaam: Open University of Tanzania.

Ndumbaro, E. (2013), "Fasihi Simulizi ya Kiafrika" Imetolewa Kutoka Chomboz Blogspot.com.

Ndungo, C.W. (1991), *Kiswahili studes* Nairobi, University of Nairobi.

Ngole. S. na Henero N. (2006),*Fasihi Simulizi ya Mtanzania,Methali Kitabu cha Pili* Dar es salaam Pres.

Njogu na Chimerah R. (1999), Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu Nairobi Jomo Kenyata Foundatio.

Njogu, K. na Chimerah, R.(1999*), Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Faundation.

Nyamsende, J. C. (2012),"Usawiri wa Taswira za Wahusika Wanyama Katika Ngano za Waikzu".Dares-salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ogechi, N. O., na Simali, k. I. (2008*), Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*.Eldoret Moi University Pres.

Okpeho.I (1972) The Study of Oral Literature. Bloomington and Indian Nopolish. Indians: University Press.

Omar, M. H. (2013), "Nafasi ya Hadithi Simulizi Katika Kufunza Maadili Mema Shule za Upili visiwani Zanzibar".Tasnifu ya Uzamivu, Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Panner, S. R. (2004),*Research Methodology* PHI Learning Private Limited,New Delhi.

Richard, M. na Wafula, R. M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*,Jomo Kenyata Foundation, Nairobi Kenya,Enterprise Road Indusrial Area.

Sengo, T. S. Y (2009), *Sengona Fasihi za Kinchi*. Daresalaam: Aera Kiswahili research Products.

Sengo, T. S. Y. (1998), Kiswahili na Uisilamu Afrika Mashariki Professorial Inaugurallectures,Mbale Islamic of Uganda.

Sewangi, S. S.and Madumulla J.S. (eds) (2007*), Makala ya Kongamano la Jubilee* ya TUKI (OL,1 and 11) Daresalaam.

Silau, A. (2013),"Tathmini Kuhusu Dhima ya Nyimbo, Katika Kukuza na Kuimarisha Malezi Katika Kabila la Wakaguru".Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Steere, E. (1970*), Swahili Tales and as Told by Native of Zanzibar*, London,Harverd College Library.

Taasisi ya Elimu Tz(1996*) Kiswahili Kidato cha Kwanza Kitabu cha Mwanafunzi* Dar es salaam,Dar es salaam: Oxford University Pres.

TAKILUKI (1981), *Misingi na Nadharia ya Fasihi,*Swiden: Berlings Arlovs.

TAKILUKI (1982),*Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar: Tanzania Publishing House.

TAKILUKI (1983*), Fasihi Simulizi Zanzibar*, Tanzania Publishing House.

Timammy, R.(1990), "Uhakiki wa Ngano za Kiswahili", Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

TUK(2004*), Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. East Africa Ltd:Oxford University Press.

TUKI, (1983)," Utafiti wa Fasihi Simulizi" Katika Makala ya Semina ya Kimataifa na Waandishi wa Kiswahili.111:Fasihi Daresalaam.

Wafula, R. M.na Njogu, K (2007*), Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*,Nairobi: Sai Industries Ltd.

Wamitila (2008), *Kazi ya Fasihi Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Videmuwa Publishers ltd.

Wamitila, K. W. (2002*), Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*, Mombasa: Phoenix Publishers Ltd.

WWW.gafkosoft.com\swa\hadithi (2009-2014).

# VIAMBATISHI

## Kiambatishi namba 1

Maswali yaliyoulizwa wakati wa kukusanya data

1) Hadithi hii mara nyingi hutolewa katika msimu gani? Mfano msimu wa mavuno ya karafuu,mpunga nakadhalika.
2) Kwa uono wako hadithi hii inatoa ujumbe gani?
3) Je hadithi hii ina dhamira gani kwa watoto katika jamii hii ya kipemba?
4) Unaweza kuniambia dhamira ambazo tunazipata katika hadithi uliyonisimulia?
5) Ni ujumbe gani ambao tunaweza kuupata katika hadithi hii?
6) Hebu niambie hapo zamani hadithi hizi hapa penu kwa kawaida zilikuwa zinatabwawakati gani?
7) Na kwa nini zilikuwa zinatabwa wakati huo ?
8) Je kulikuwa na athari gani iwapo mtu atavunja mwiko na akazitamba wakati wowote anaopenda yeye?
9) Katika jamii hadithi hizi zinaendelezwaje ili zisipotee na hasa katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia?
10) Katika zama za leo hapa penu watoto wanapata nafasi ya kusimuliwa hadithi hizi za kijadi za paukwa ----pakawa?
11) Je watoto wenu katika kijiji chenu wanatambiana hadithi wao kwa wao ?
12) Hadithi hizi za paukwa pakawa katika jamii yenu zilikuwa na dhima gani?
13) Je hadithi hizi za watoto zina nafasi gani katika kufunza watoto?
14) Je unaweza kunipatia watoto watano ambao wanaweza kunisimulia hadithi hizi za paukwa ----pakawa?
15) Naomba unitafsirie hadithi hii kwa Kiswahili sanifu
16) Naomba unitafsirie nyimbo iliyomo katika hadithi uliyonitambia.

**Kiambatishi namba 2**

**Hadithi ya kwanza Zimwi**

Paukwa…………………….pakawa

Hapo zamani za kale walikuwepo Makame wa Makame na Mboje,watu hawa walioana na wakazaa watoto wawili Mize na Pate. Pate aliolewa na baadae akamchukuwa Miza kumlea, mume wa Pate alipokuja kumposa Pate wazee wake walikataa lakini Pate alishikilia hadi wazee wake wakakubali.Miza wakati akiwa kwa dada yake alikuwa na kawaida ya kumpelekea shemegi yake chakula,Miza alipofika shamba alimwita shemegi yake kwa sauti "muwamu weee muwamu weee"alimwita mara tatu,na shemegi akaitikiya "naam muwamu moto shima shima nimuitikie muamu".Miza alimpa shemegi yake chakula kisha akaondoka.

Siku nyengine Miza alikwenda tena kumpelekea chakula shemegi yake, alipofika karibu na shamba alimwita shemegi yake kama kawaida yake na shemegi nae akaitikia vilevile na huku akiwa kaota mkiya na unawaka moto nyuma.Baada ya siku kadhaa kupita Miza aligunduwa kuwa shemegi yake alikuwa ana mkia unaowaka moto mithili ya mwenge wa kurambazia madodo,kwa hivyo akajuwa kuwa shemegi yake alikuwa zimwi.Baada ya kugunduwa hivyo, alikwenda kumwambia dada yake Pate kuwa mume wake ni zimwi na ikiwa hamuamini siku moja atakapokwenda kumpelekea chakula wafuatane ili akamshuhudize kwa macho yake.

Siku iliyofuata, Pate aliongozana na dada yake kwenda kupeleka chakula shambani na kama kawaida yekewalipofika Miza akamwita shemegi yake"muamu weeee muwamu weeee" na shemegi akaitikia", naaaam muamu moto shima shima nimuitikie muamu,Mize akamwambia dada yake asogee amsikilize asemavyo na kisha amuangalie nyuma ili auone mkia unavyowaka moto huku ukilalama. Baada ya kuona hivyo

aligunduwa kuwa mume wake nizimwi na akagunduwa kuwa kuna siku atakuja kuwala, kwa hivyo wakaamuwa kukimbia na kurudi kwao.Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya pili ya Chura na Jongoo**

Hadithi; hadithi……hadithi njoo utamu kolea.

Hapo zamani za kale alikuwepo chura na jongoo,wanyama hawa walikuwa marafiki wakubwa,siku moja chura aliingiwa na uchoyo mkubwa kwa kumuona rafiki yake jongoo anameremeta sana,na mara akamuuliza,rafiki yangu unafanya nini hadi unameremeta kiasi hicho.Jongoo kwa mapenzi akamjibu,unachukuwa maji yako unayateleka,lakini kabla jongoo hajamaliza chura akamdakiza na akamuuliza ukaruka ukaingia mumo? Jongoo akamjibu hata huingii, Jongoo akaendelea ukisha yateleka,lakini pia kabla hajasema akamaliza chura akamdakiza tena ukaruka ukaingia mumo? Jongoo kwa hasira akamwmbia hee! Hebu nipishena huku jongooakiondoka. Lakini chura kwa madaha akasema,kama ulikuwa hutaki nijuwe siri ya kumeremeta kwako, basi leo nimeshajuwa.Chura nae akaondoka,akenda nyumbani kwake kroo! Kroo! Kroo! alipofika akateleka maji,yalipokuwa tayari yanachemka chura akajirusha ndani ya sufuria,kitu ambacho kilimsababishia kufanya madonda mwili mzima na alipopowa ngozi yake ikawa na mafurungu furungu.Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi yaTatuya Makame wa Makame.**

Paukwa………pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo Makame wa Makame.Bwana huyu alimuowa mke wake aliyeitwa Mboje.Makame wa Makame aliishi na mke wake vizuri.Lakini baada ya muda mke wake alifarikikwa ugonjwa wa ndui. Baada ya mke wake kufariki, Makame wa Makame alihama katika kijiji alichokuwa akiishi na mke wake Matumbini na akahamia

anakoishi mama yake katika kijiji cha Upo.Watu wa kijiji cha Upo walikuwa ni wavuvi, kwa hivyo Makame wa Makame nae akajiunga nao. Siku moja, akamwambia mama yake kuwa na yeye anakwenda agoni kuvua.Mama wa Makame kwa vile huyu alikuwa ni mtoto wake wa pekee, alikataa sana mtoto wake kwenda kuvuwa agoni. Lakini baadae alikubali na akamwambia basi mwanangu nenda salama.Makame wa Makame alifurahi sana,na akamwambia mama yake sawa, lakini nakupandia mpachori huu, ukiuona unanawiri ujuwe na mimi niko vizuri na mzima wa afya, lakini ukiuona unanyauka ujuwe na mimi afya yangu sio nzuri au nimeshafariki.Mama alikaa kwa muda mpachori ukawa unastawi vizuri lakini baadae mpachori mara ukaanza kunyauka.Mama akawa na wasiwasi na akateremka bwachini. Aliwaona baadhi ya wavuvi wanarudi kuvua na akawauliza kwa kutumia wimbo.

"Hujanionea mwanangu Makame ilenge,

Hujanionea mwanangu Makame ilenge"

Na wale wavuvi wakamjibu kwa wimbo.

"Namuona wakati wa kuja, namuona wakati wa kuja

ufataufisa Makame nyuma yuaja".

Mama aliuliza kuanzia kidau cha kwanza hadi cha saba. Kidau cha saba alijibiwa hivi:

"Namuona wakati wa kuja, namuona wakati wa kuja.

Ufataufisa Makame, kashajifia.

Makame aletwa kwao."

Mama alilia sana baada ya kuambiwa kuwa mwanawe ameshafariki.Mama alilia hadi akapofuwa macho. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya nne ya Paka na Panya**

Paukwa……pakawa.

Hapo kale alikuwepo Paka na Panya, wanyama hawa walikuwa marafiki sana ikawa kila kitu wanafanya kwa pamoja, lakini walikuwa hawana makazi maalumu na walikuwa wakitangatanga tu.Siku moja Paka akamwambia Panya wajenge nyumba, ili wapate sehemu ya kuishi. Panya alikubali na wakaanza ujenzi.Lakini kumbe katika ujenzi wao Panya alikuwa amekusudia kumfanyi ujanja Paka kwa vile yeye ndie aliekuwa fundi mkuu. Nyumba hile aliitia mlango mdogo mno, kiasi ambacho paka alikuwa hawezi kupita. Mara baada kumaliza nyumba hiyo  Panya akamwambia paka aingie ndani,lakini kutokana na mlango kuwa mdogo mno Paka alishindwa kuingia ndani.Aliposhindwa kupita paka alimwambia panya aanze kuingia yeye. Panya alipoingia aliingia kinyumenyume(alianza kuingia mkia) kufika katikati Panya akakwama,kwa hivyo Paka kuona hivyo akamwambia, Paka rafiki yangu nimekwama naomba msaada wako, nivute. Paka alikataa na Panya akaanza kulia chwiii! Chwiii.

Paka akamwambia kunaambiwa ninani upenyeze mkia, baada ya muda Paka akamla Panya na hadi leo Paka na Panya ni maadui.

**Hadithi ya tano ya Sungura.**

Hadithi…hadithi!

Hadithi njoo!

Hapo zamani za kale, alikuwepo Nfaki na watoto wake wawilina mke wake,waliishi katika mtaa wa wa Mbaoni,Nfaki alikuwa ni mkulima wa mazao mbalimbali katika shamba lake,shamba hilo lilikuwa mbali kidogo na kule anakoishi.Siku moja Nfaki alimtaka rafiki yake wa siku nyingi, kuja kumtembelea nyumbani kwake. Kwa vile walikuwa hawajaonana siku nyingi. Asubuhi ilpofika walipanga yeye na mke wake

maandalizi mazuri kwa ajili ya mapokezi ya mgeni wao na kumuandalia chakula kwa wakati atakapokuwepo.

Katika maandalizi hayo walimuandalia kitoweleo cha Jogoo mkubwa. Nfaki alitoka yeye na watoto wake wawili kwenda shamba ilikutafuta mazao kwa ajili ya zawadi za mgeni wao. Walipofika shambani walimkuta Mzee Sungura akiwaibia mazao yao. Nfaki kwa hasira alizokuwa nazo aliwambiya watoto wake wamchukuwe wampeleke kwao na aongezewe kwenye chakula cha mgeni. Walipofika njiani Sungura akawageukia watoto na akawazidi akili kwa kuugeuza ujumbe walioagizwa na baba yaO,na akawambia mumeambiwa na baba yenu mukamwambie mama yenu huyo mgeni ndie mimi na hivyo vitu vyote alivyoandaliwa mgeni nipewe. Kwa vile watoto walikuwa wadogo walikubali na wakadhani huwenda wao wamesahau na Sungura ndie aliyesema kweli.

Kwa hivyo Sungura alipofika nyumbani aliandaliwa kila kitu ambacho aliandaliwa mgeni.Baba yao aliporudi kuingi ndani alimuona sungura yumo ndani kaka juu ya mkeka,na pale alipokuwa kakaa alikuwa kashachimba shimo bila ya kujuilikana, shimo hilo lilikuwa limetokeza nje ya nyumba.Nfaki alipoingia jikoni alimgomba sana mke wake na akataka ampe sababu kwa nini akamuacha Sungura hadi sasa akawa bado anaishi.Aliporudi ukumbini alitaka kumuadhibu Sungura lakini alikuwa ameshakimbia kwa kupita katika lile shimo alilolichimba.Na hadithi yangu ikaishia hapa.

**Hadithi ya sita ya Fisi na Simba**

Hadithi hadithi!

Hadithi njoo

Hapo zamani za kale alikuwepo Simba, Simba alikuwa ndie mfalme,wanyama wote walimuheshimu, katika kijiji chao kulikuwa na shida kubwa ya maji,ili kutatuwa tatizo hili,Simba aliona bora awashauri raia wake wachimbe kisima,wanyama wote walikubali isipokuwa Fisi akakataa kwa kutaka apate chake peke yake, Fisi alisema yeye hataki kuchimba kisima cha ushirika na badala yake atachimba kisima chake peke yake.Wanyamawengine waliosimamiwa na Simba walichimba kisima na wakawa wanachota maji safi lakini Fisi yeye alishindwa na akawa hana pa kuchota maji. Kwa vile Fisi alikuwa hana pa kuchota maji ilimbidi akaibe maji katika kisima cha ushirika wakati wa usiku, wenyewe walimuona na walimkamata wakapiga bakora.Na hadithi yangu ikaishia hapa.

**Hadithi ya sabaya Kungu Mauwa.**

Paukwa…………….pakawa.

Hapo zamani za kale mtu na mkewe, mke aliitwa Mwau na mume aliitwa Lau.Nyumba yao ilikuwa na vyumba saba, lau alimwambia mke wake, vyumba vyote funguwa isipokuwa chumba cha saba tu usifunguwe. Siku moja shangazi wa Mwau alikuja kumtembelea Mwau nyumbani kwake, alipofika alibaini kuwa Mwau ana chumba kimoja katika nyumba yake hakifunguwi na akamuuliza kwa nini hakifungui chumba hicho, nae Mwau akamjibu kuwa kakatazwa na mume wake.Shangazi alichukia sana aliposikia hivyo na akamshawishi Mwau,ingawa alikataa sana na shangazi yake akamwambia “eee” mtoto wewe akwambiaye akupenda hujihumo chumbani muna nini huwenda muna mali mume wako enda honga wanawake wengine nje na wewe utabaki hivyohivyo nan a ujinga wako huo. Mwau akakubali kukifunguwa chumba cha saba,Mwau alipokifunguwa ndani aliliona jini linameremeta sana lina vichwa saba, Mwau aliogopa sana na akataka

kukimbia lakini jini lilimwambia usikimbie, nifungulie mlango nitoke, kwa hofu Mwau aliufunguwa tena mlango jini likatoka likenda mtoni,mume wake aliporudi kazini, mara baada ya kuingi ndani aligunduwa kuwa mke wake chumba cha saba kalifunguwa na jini lake limeshakimbia,kwa hiyo alimgomba sana mke wake kwa kuvunja amri zake.Kisha akamwambia kuwa wewe hujui kama mimi hilo jinni nilikuwa ninalitumia kwa kuchumia mali, kwa hivyo nataka utoke sasa hivi wende ukamtafute kungu mauwa wangu (jini) na umrejeshe mule mule alimokuwemo katika chumba cha saba.Mwau alitoka akenda hadi mtoni, akakuta maji yanameremeta,akajisemea peke yake, huyu itakuwa ndie kungumauwa, na akaanza kuimba,

"Ni wewe kungumauwa, ni wewe kungu mauwa,

Nitumwa tumwa ni bwana,wewe nije kubeba,

Na nyumbanimo ukangie, weee kungumauwa"

Yule mume wa Mwau alikuwa kapanda mti mrefu kwa hivyo alikuwa akimuona mke wake kila alipokuwa akipita wakati akimtafuta kungumauwa, Mwau alipombeba yule kungumauwa (jini).alipokaribia nyumbani mume wake alimwambi mrudishe! Mrudishe! Huyo sie.Mwau alimrejesha kulekule mtoni.Akenda mto wa pili akamuona mwengine, aikaambiwa amrejeshe na huyo sie, akenda hadi mto was aba ndio akamkuta akamchukuwa akenda nae na mume wake akafurahi sana.

Baada ya siku tatu Lau alimwambia mke wake wakawatembelee wazee wa Mwau, na kama kawida Mwau alifurahi sana, na wakajiandaa wakatoka wakenda hadi kwao pamoja na mume wake.Walipofika walipokewa na kukaribishwa vizuri wakachinjiwa kuku jogoo mkubwa kwa ajili ya itoweleo. Walipomaliza kula walitembelea ndugu wengine pale kijini pao na baadae wakarudi tena kwao Mwau.Lau aliwaita wazazi wa Mwau na akaweleza makosa yote ya mwanawao Mwau, na alipomaliza akwambia kuwa yeye kwa kosa hilo ameshamuacha.Nadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya naneya wake wenza.**

Hapo zamani za kale alikuwepo bwana Jape na wake zake wawili, mmoja Bi Kikulccho na mwengine Bi Maonevu, wanawake hawa walioneana wivu kupita kiasi kwa mume wao, kila mmoja alitaka mwenzake aachwe ili abakie yeye peke yakekwa bwana jape. Mke wake mdogo Bikikulacho alikuwa na motto mmoja tu wa kike, na mke wake mkubwa Bimaonevu alikuwa na watoto watatu,wa kike mmoja na wa kiume wawili.

Siku moja mototo wa Bikikulacho alimwambia mama yake wa kambu amtengenezee kijungu na mkungu, (wa udongo), Bimaonevu akamwambia ikiwa unataka nikutengenezee basi muuwe mama yako,kwa kumsukuma kwa kumtia kisimani atakapokwenda kukuogesha.Mtoto alikimbia mbio hadi kwa mama yake mzazi na kumuomba mama yake wende kisimani akamuogeshe. Mama alikubali, lakini walipofika kisimani wakati mama yake alipokuwa akichota maji mtoto alikwenda akamsukuma mama yake (Bi kikulacho) akaingia kisimani na akafariki.Mtoto alipoona vile alirudi mbio hadi kwa mama yake wa kambu huku akiimba.

Kunambili, nintie nvyele kisimani

Unipatili, kijungu na nkunguani.

Nintili mbali, kajifia mbali

Mtoto alipofika kwa mama yake wa kambu akamkejeli kwa kumwambia nyoo kushamuuwa mama yako kwa kijungu na mkungu, “ama kweli kikulacho kinguoni mwako”,jina la mama yako lilimsibu, nenda huko.Nakuanzia hapo mototo huyo akawa anateswa na mama yake wa kambu, hapewi chakula akashiba, yeye alikuwa ndie mfanya kazi zote za ndani, mtoto alikonda sana,na baba yake akiuliza mbona Makidi anakonda sana Bimaonevu anamwambia ana fikira tu huyo za kufiwa na mama yake, kumbe alikuwa hapewi chakula akashiba.Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya tisa ya Yamuimui.**

Paukwa……………………. Pakawa

Hapo zamani za kale walikuwepo wanakijiji, mwanakijiji mmoja alizaa mototo mzuri sana, mtoto huyo alikuwa akiitwa Yamuimui, pale kijijini kila mtu alikuwa akimsifu Yamuimui kwa uzuru wake,kitu ambacho watoto wenzake kiliwachukiza sana.

Siku moja watoto walipanga kumuuwa Ymuimui, walikwenda hadi kwa mama yake wakamuomba ili amruhusu wende wakacheze na kuvuwa kombe bwachini, kwa bahati mama yake Yamuimui alikubali na wakaondoka nae wakenda nae mwituni, kisha wakamwambia, sisi mtaani hatuna raha kwa sababu yako eti kwa kuwa umzuri sana, sasa leo tunataka tukuuwe ili hili balaa lituondokee angalau na sisi tupumzike kubuguziwa kwa sura zetu mbaya.Walipokwisha kumuuwa wakampachika juu ya panda ya mti na wao wakarudi zao majumbani kwao.Mama yake Yamuimui alipoona muda umekuwa mkubwa akaona bora akawaulize watoto wenzake Yamuimui yuko wapi mbona hajarudi nyumbani? Watoto wakamjibu sisi hatujui maana tumerudi nae zamani na tumemuacha anakwenda nyumbani kwao.

Mara mama baada ya kuondoka tu alifuatwa na mbwa na akawa anabweka sana, na kasha mbwa akaimba;

Yamuimui…Yamuimui
kapachikwapanda ya mti kulee kulee
watu wende nami nende nikasikize kilio
Yamuimui kauwawa.

Baadhi ya watu wakasema, jamani tumfuateni huyu mbwa huenda ikawa kaona jambo, kwa hivyo baadhi ya watu wakamfuata mbwa na mbwa akenda mpaka iliko maiti ya Yamuimui na hapo watu wakajuwa kuwa Yamumui kauwawa. Akachukuliwa akenda akazikwa Na hadihi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya kumi ya Bunuwasi.**

Paukwa…………pakawa…… mwana wa kasa mpasha mwanao na mwana wa mwenzio ndio mji ukavuma.

Hapo zamani za kale alikuwepo bunuasi na wanakijiji, watu hawa walichimba kisima chao wakawa wanatumia kwa kuchota maji, lakini Bunuasi akawa na tabia ya kuchota maji, akishajaza vyombo vyake maji huyachafua yakawa machafu.watu wakija asubuhi wanasema kuwa huyu aliyeyachafuwa maji ni bunuasi,laikini Bunuasi akakataa sana, wanakijiji wakapanga kumtega mbaya wao, kwa umoja wao bila ya kumshirikisha Bunuwasi wakatengeneza mtu kwa kutmia urimbo (utomvu wa mbungo),akawa na miguu, mikono,kama mtu.

Siku moja wakenda wakamuweka kisimani usiku bila ya kumvisha nguo, kwa hivyo bunuasi alipokwenda kuchafua maji hakumjua kuwa sio mtu,aliona ni mlinzi tu,kwa hiyo akamwambia wewe ndio unajifanya mlinzi, basi mimi hunishughulishi nitakupiga kibao kimoja tu, akampiga akanasa makono wa kwanza,akamwambia aaaa! Kwani mkono wa sinao? Akampiga akanasa mkono wa pili, akamwmbia aaaa! Kwani mateke hayapo?akampiga akanasa miguu yote miwili, akamwambia aaaa! Kwani kichwa sinacho?Akampiga kichwa nacho kikanasa. Kwa hivyo Bunuasi akanasa hadi asubuhi, akakamatwa na ikaamuliwa akatupwe baharini makondoni. Lakini kabla ya kutupwa aliomba bora atiwe katika sanduku ili azame harakaharaka. Ombi lake hilo lilikubaliwa na akachongewa sanduku akaingizwa,mara kulitokea mtu anaumwa watu wote wakashughulika na yule mgonjwa na Bunuasi akaachwa peke yake lakini yumo ndani ya sanduku,mara akatokea mgunya anaua urembo akauliza mna nini humu ndani ya sanduku nimo mimi nimejificha natakiwa nimuowe motto wa mfalme na mimi simtaki, mgunya kusikia vile akasema basi toka niingie mimi kisha nitasema kuwa namtaka na wewe

chukuwa huu urembo wangu wende ukauze maana mimi nikisha kumuowa mototo wa mfalme nitakuwa tajiri.

Bunuasi alikubali na akatoka katika sanduku akaingia Mgunya.Mara baada ya kumfungia Mgunya sanduku Bunuasi alikimbia bila ya kuonekana na mtu, na watu waliporudi wakalibeba sanduku wakalipeleka baharini katikati ya mkondo wakalitupa na yule mgunya akafariki.

Baada miaka kadhaa, Bunuasi alirudi tena kijijini pao na watu wakamshangaa sana kwa vile walijuwa ameshafariki, laikini aliwambia mimi huko nina raha sana na akawambia wale waliofiliwa wazazi wao kuwa wazazi wao wanawasalimia na karibu atarudi kwa hivyo aliye na zawdi ya kumpelekea mzee wake ampe awapelekee.Watu walikusanya zawadi mbalimbali wakampa Bunuasi azipeleke na Bunuasi akaondoka nazo akenda kuziuza ukooo Mizemiumbi, akatajirika na akawa anawadharau sana watu wa kijijini pao kwa kuwaita majuha. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya kumi na moja ya watoto saba.**

Paukwa……………….Pakawa

Hapo zamani za kale alikuwepo mtu na watoto wake saba,sasa baba yao siku moja alikuja mgeni mtaani pao,alikuwa ni mgeni wa jirani yake,sasa akamwambia aaa! Nataka nipate mwalimu anisomeshee wanangu,yule mgeni alimwambia mimi ni mwalimu kwa hivyo nipe tu nitawasomesha lakini niletee mmoja mmoja usiwalete kwa pamoja.yule baba wa watoto saba akakubali na alipoondoka akamchukuwa yule mkubwa wa mwanzo.Lakini kabla hawajafunga safari yule mwalimu alisema wafanyiwe mikate saba kila mmoja kwa sababu wanakokwenda ni mbali mno, kwa hivyo walipikiwa mikate, wakapwa na kibirika cha maji kila mtu chake kasha wakaondoka.Wakenda wakenda

wakenda weee ata ukoo mwalimu akasema sasa towa mikate yako tuile,yule mtoto akaitoa wakila yote .

Wakaendelea na safari yao tena,msitu na yika msitu na nyika mpaka ukooo mwalimu akasema sasa natoa mikate yangu nakula, na wala sikupi sio yakokushayali, mtoto akawa hana la kusema akmtazama tu, kasha wakaendelea na safari yao lakini mtoto ana njaa kali.

Wwalipokaribia nyumbani kwa mwalimu, mwalimu alimuonesha mtoto miti mbalimbalina kila mmoja akawa anamfahamisha huu ni dawa ya kitu Fulani na huu ni dawa ya maradhi Fulani,kwa ujumla alimfundisha dawa za maradhi mengi sana kitu ambacho kilimfanya awe daktari mzuri sana pale kijijini pao.Walipofika nyumbani kwa mwalimu, wakati wanataka kua chakula,mwalimu alilalama tumbo linauma na akamtaka mwanafunzi wake akamchumie dawa ya tumbo kule walikopita na akamuonesha dawa, mtoto aliacha kula pamoja na kuwa alikuwa na njaa kali akenda kumchumi mwalimu wake dawa. Mtoto aliporudi alikuta chakula chote mwalimu wake ameshakila na jikoni hakiko tena, lakini mtoto aliendelea kustahamili njaa ili apate elimu.

Baada ya siku kadhaa mtoto alirudi kwao akiwa na utaalamu mkubwa wa tiba za magonjwa ya binadamu. Aliporudi alimshawishi na mdogo wake nay eye ende ili akasome kama yeye, kwa bahati nzuri siku ya pili tu mwalimu alifika na akaondoka nae. Njiani alimfayia kama aliyofanyiwa kaka yake,ya kuwekwa na jaa lakini yeye hakuweza kustahamili,alipoona njaa ni kali mno akaamuwa kumkimbia mwalimu na akarudi kwao kwa hivyo kusoma kukamshinda ktu ambacho kiliwavunja moyo na wale waliobakia nao wakasema nasisi hatuendi inaonekana huyu mwalimu ana upedneleo kwa nini kaka yeye alimpa elimu mpaka akahitimu lakini wewe anakuweka na njaa tu.

Kaka yao aliwambia na mimi alinifanyia hivyo hivyo nilivumilia tu, wewe ndio hamuwezi kuvumilia au ndio ukubwa ni jaa? Na hadithi yangu ikaishia papo.

**Hadithi ya kumi na mbili ya Babu Dii**

Hadithi…………….Hadithi

Hadithi njoo…………utamu kolea

Hapo kale alikuwepo babu dii na mke wake na watoto wao saba,watu hawa walikwa maskini sana hata chakula chao kilikuwa cha tabu. Siku moja babu dii aliwaza sana kuhusu kupata kazi ilia pate pesa akanunuwe chakula,akaona ni bora aende nje ya kijiji chao akatafute kazi, akendaakena mpaka ukoo akuta msitu mkubwa lakini kwa mbali akaona kuna sehemu kunafuka moshi, akasema lazima nifike kule kunakofuka moshi, akenda akenda akenda hata hukoo akafika, akaona kijibanda kidogo, mara kikatoka kibibi kikongwe,kikamuliza, mjukuu wangu unakwenda wapi huku hakuji mtu isipokuwa awe na hisa miongoni mwetu, Babu dii akamwambia nimekuja kutafuta kazi, akamwambia kama unataka kazi njoo nikupe, babu dii akenda akachukuliwa hadi kibandani na bibi akamwambia kama wataka kazi kwanza nirambe tongo zangu zote mpaka zimalize,niweze kuona vizuri. Babu dii akamramba tongo bibi mpaka zikamaliza nabibi akawa anaona vizuri. Baada kumaliza babu dii alipewa pesa na mapande matatu ya dhahabu akayauze apate pesa zaidi ili aanze biashara yake mwenyewe, Babu dii akaondoka, akarudi kwake na mali zake na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya kumi na tatu ya Kijoka.**

Paukwa …………………………..Pakawa.

Hapo zamani za kale alikuwepo mama mmoja ambae alikuwa hajapata mototo, siku moja mama huyu alikwenda kutafuta kuni, akaona gogo akalichanga, mara akatoka nyoka,

mama akasema heee! Angalau na mimi mungu angenijaalia nikazaa mototo japo kama hichi kijoka. Yule mama alikaa kwa siku nyingi mpaka akasahau kuwa aliomba mtoto, kwa bahati mama akabeba ujauzito na akazaa kijoka cha kiume, yule mama akafurahi sana kwa kupata mtoto, akamlea mpaka akafikia umri wa miaka saba,siku moja akamtuma yule mtumishi wake anaemshughukilikia, na akamwambia kwa wimbo;

Kanu wangu kanu wangu; kanu

Nednda kamwambie mama; Kanu

Kuwa kijoka ataka tohara, Kanu

Kwa kusika hivyo Kanu akenda akamwambia mama yake kijoka kuwa mwanawe ataka tahiriwa, kwa vile mama alikuwa na uwezo mkubwa na mali nyingi akampa yaya kinu na mchi wa dhahabu apige upatu atakaemtahirimwanawe atapewa hicho kinu na mchi wa dhahabu.

Ilikuwa kila apitapo watu wanamkejeli kwa kusema sitafuti kuja nikatafunwa ni nyoka mimi. Lakini baada ya kuzunguka sana, alitokea bwana mmoja mzee kidogo akasema mimi nikwenda kumtahiri kwa hivyo akenda kumtahiri akapewa kinu na mchi.

Wakakaa hata baada ya muda kijoka akamwambia Kanu.

Kanu wangu Kanu wangu ; Kanu

Nenda kamwambie mama ; Kanu

Kuwa kijoka ataka mke; Kanu.

Kanu akenda kwa mama yake kijoka akamwambia kuwa kijoka ataka mke.

Mama akasema haya, akamwita yaya akamwambia apige mbiu ya mgambo atangaze kuwa atakae kubali kumuolewa na kijoka atapewa pesa nyingi na jumba kubwa la kifahari. Mbiu ilianza lakini kila mtu aliesikia alisema aaaa! Nimpe mwanangu kijoka aje amtafune, sifanyi kosa hilo, lakini mwisho wa mji tena akatokea mwari mmoja akasema

mimi namtaka hata kama ni kijoka, akamwambia mama yake achukuwe zile mali ili watokane na umaskini mkubwa walionao nay eye akaolewe na kijoka.

Kwa hivyo wazee wa yule mwari wakenda wakamuozesha kijoka mototo wao lakini walikuwa na hofu ya mtoto wao kuliwa na kiloka,lakini kwa vile ni maskini sana wakaona basi nawamuombe Mungu tu.Kumbe yule kijoka alikuwa si nyoka bali alikuwa ni mvulana mzuri sana wa kiarabu,kwa hivyo mke wake akagunduwa kuwa mume wake alikuwa ni mtu kamili na mume wake akamtaka asimwambie mtu kuwa yeye si nyoka.

Walikaa siku nyingi,baadae siku moja akamwita Kanu na akamwambia;

Kanu wangu Kanu wangu; Kanu

Nenda kamwambie mama Kanu

Kijoka atoka nje; walimwengu wamuone.

Aeee! Kanu walimwengu wamuone.

Kanu akenda kwa mama yake akamwambiya kuwa kijoka ataka kutoka nje, mama yake akaona huu sasa mtihani, mwanangu hatauliwa, akaona bora amkataze asitoke lakini kijoka akasema bora nitoke. Huko nje watu wakaambiwa, lakini wakaona wajilinde kwa hivyo watuwakakaa na mapanga, mashoka na marungu wataka muuwa kijoka.

Mara kijoka akatoka na mke wake wakiwa wamependeza na wakamuona kuwa sio nyoka bali ni mtu mzuri,watu wakashangaa na zile silaha zao zote wakazitupa chini, na wakabaki wanalalamika kuwa walidanganywa kumbe si nyoka nitu mzuri tena mwenye mali. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi ya kumi na nne ya mtu na ndugu yake.**

Paukwa………………………Pakawa.

Hapo zamani za kale walikuwepo ndugu wawili, Ali na Juma, Ali alimpenda sana ndugu yake, lakini Juma hakuwa na upendo mkubwa kwa kaka yake, alimjali sana rafiki yake kuliko kaka yake. Siku moja kaka (Ali) alimwita ndugu yake Ali na akamwambia, ndugu yangu duniani ukikaa ni vyema rafuki yako wa kweli awe ni ndugu yako w damu, kwa sababu ndie mutakae kaa na kusaidiana. Juma alikataa mawazo ya kaka yake na kamwambia mimi siwezi kuacha kushirikiana na rafiki yangu mpenzi wa tokea enzi na enzi nikakufuata wewe kwani wewe huna marafiki zako ukashirikiana nao.Juma akazidi kumsisitiza ndugu yake, eee! Ndugu yangu rafiki hazoi mbwambwa azowa kavu, mimi ni kaka yako na nimekubali kuwa wewe ni ndugu yangu sikukatazi kuwa na rafiki lakini na mimi kaka yako nataka unijali na tushirikiane kwa raha na shida, lakini Juma bado akashikilia msimamo wake na Ali akambia sawa ndugu yangu utakuja nikumbuka pindi mwakani.

Watu hawa waliishi kwa muda, siku moja Juma akenda baharini kuvuwa akapata samaki mkubwa sana, na kwa vile ilikuwa usiku akasema bora nenda kumuamsha rafiki yangu aje anisaidie kumbeba maana peke yangu simuwezi, lakini wakati akiwa anamvuwa yule samaki, ilimbidi ampige mapanga ili kumunguza nguvu asije akamjeruhi, kwa hivyo Juma alijaa damu ya yule samaki akawa kama aliyechinja mtu na akarukiwa na damu. Alipokwenda kumuamsha rafiki yake alipotoka akamuona karowa damu akaufunga mlango kwa kasi na akamwambia aaaa! Mimi sitoki humu, tena toka toka mimi usinitafutie matatizo kushauwa huko wanijia mimi nikusaidie, nikusaidie nini, aaaa! Huna kazi we.Hebu nenda.

Juma alipoona rafiki yake kamrusha,akakumbuka maneno ya kaka yake, akasema ama kweli alivyonambia kaka ni kweli, lakini basi bora nikamuombe radhi kaka yake na ikisha amuombe akamsaidie kumbeba samaki hadi nyumbani kwake. Alipofika kwa kaka yake, alimgongea mliango akmwambia ni mimi ndugu yako Juma, hakumdidisi tena bali

alitoka na akamwambia vipi ndugu yangu nikusaidie nini? Akamwambia nifuate huku, Ali bila kigugumizi alimfuata pamoja na kuwa alimuona karowa damu lakini alijua kuwa tatizo lolote lililomkuta litakuwa lao wote kwa hivyo akaona haina haja ya kumuuliza kafanya nini hadi akarowa damu kiasi kile, wala hakujali kama pengine kauwa na takwenda kumtia matatizoni.Ali alimfuta hadi bandarini na walipofika wakamchukuwa samaki wakampeleka nyumbani kwa Juma,asubuhi ilpofika Juma alimwambia kaka yake,ama kweli kaka yangu mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe, nimethibitisha maneno yako,na kuanzia leo mimi rafiki wa kweli ni wewe ndugu yangu.Na hadithi yangu ikaishia hapa.

**Hadithi ya kumi na tano ya Muhamedi.**

Paukwa………………………..Pakawa

Hapo kale alikuwepo mama mmoja na watoto wake saba lakini baada muda yule mama akamchukuwa mototo wa kulea,mtoto huyo aliitwa Muhamedi, mototo huyo alipendwa sana na yule mama, wale watoto wakajuwa kuwa mama yao anampenda sana Muhamedi kuliko wao,siku moja watoto wakapanga kumuuwa Muhamedi ilimama yao awapende wao kwa vile Muhamedi atakuwa kashafariki.

Baada ya siku kupita watoto walimsubiri mama yao katoka kwenda shamba wakamwambia Muhamedi wende wakatege ndege msituni,Muhamedi alikubali na akawafuata kaka zake wakenda kutega ndege, walipofika huko msituni wakamgeukia Muhamedi, wakachimba shimo kubwa wakamuingiza, na kumwambia kaa humo shimo likule, kwa vile Muhamedi alikuwa mdogo sana hakuweza kutoka mwenyewe ndani ya shimo, kwa hivyo wale kaka zake walipokwisha kumtia ndani ya shimo wakaondoka wakarudi nyumbani kwao na walipofika wakanyamaza kimya.

Mama aliporudi shamba akawauliza wanawe,Muhamedi yuko wapi? Watoto wakamwambia mama yao wao hawamjui alipokwenda, mama akapita kijiji chote kumtafuta lakini hakumuona,watu kijiji kizima wakashughulika kumtafuta hawakumuona, kwa hivyo wakakata tamaa, wakakaa matanga kwa kuwa Muhamedi itakuwa ameshafariki.

Kule msitini walikomtia shimoni Muhamedi, kulikuwa na kibibi kizee kilimuona Muhamedi ndani ya shimo wakati kilipokuwa kikipita karibu na lile shimo bila ya kutegemea kuwa mulikuwa na mtu, kibibi kilpomuona kilimtilia jiti kubwa kikamwambia alikamate na kupanda hilo jiti,Muhamedi alitoka na kibibi kikamchukuwa hadi nyumbani kwake na kikawa kinakaa nae nyumbani kwake.

Siku moja Muhamedi alimwambia kibibi bora wafanye biashara ya vikapu kwa sababu yeye anajuwa kusuka vikapu, kibibi kilikubali na Muhamedi akaanza kazi ya kusuka vikapu wakiuza, vikapu vilikuwa vinakwenda vikiuzwa kule kijijini kwao Muhamedi, kwa vile watu walikuwa wameshazoea kununua vikapu kama hivyo kwa Muhamedi walipoviona wakasema hivi vkapu vizuri kama vile alivyokuwa akisuka Muhamedi. Kwa hivyo watu walivinunua vyote, na sasa kibibi ikaw ndio biashara yake kila siku, baada muda kupita kuna kijana mmoja akamuuliza kibibi, hivi vikapu unatengeneza wewe au kuna mtu anakutengenezea? Kibibi kikamwambia ninae mjukuu wangu ndie anetengeneza, kijana akamwambia anaitwa vipi? Akamwambia anaitwa Muhamedi, kijana akamwambia basi leo ukiondoka na mimi nataka nije nimembelee huyo mjukuu wako, kibibi kikakubali.

Kijana nia yake si kumtembelea mjukuu wake tu bali alitaka amjuwe kwani alikuwa na wasiwasi kuwa huwenda akawa ndie yule Muhamedi waliemtafuta bila ya kumuona. Walipofika nyumbani kwa kibibi, ikjana alimuona Muhamedi na akakimbia mbio hadi kijijini kwao akapeleka habari kwa Muhamedi kamuona.

Mara baada ya kijana kutoa taaifa yakumuona Muhamedi, watu wote waliongozana na kijana hadi nyumbani kwa kibibi, walipofika kibibi aliwakaribisha vizuri na wao wakamuona Muhamedi na wakataka kumpiga kibibi kwa kumficha Muhamedi, lakini Muhamedi akawaeleza ukweli wote kuhusu waliyomfanyia kaka zake, kwa hivyo watu wakampongeza kibibi kwa kumsaidia Muhamedi, kwa hivyo wakamchukuwa kibibi na Muhamedi na wakamtaka wakaishi pamoja kijijini kwao, na wale kaka zake Muhamedi wakakamatwa wakaadhibiwa na hadithi yangu ikaishia hapo.